SportPesa
TZS. 804,667,160
NI YA KWAKO WIKI HII,
BETI LEO UWE MILIONEA
SPORTPESA.CO.TZ PIGA *150*87#



## Ajali gari la mizigo yaua watu wanne

UKURASA 5


# Nipashe Jumapili


MWANGA WA JAMII

Jumapili Desemba 26, 2021 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

www.ippmedia.com

ISSN 0856 • No. 0580806

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US


**DIAMOND, ZUCHU** lisemwalo lipo, iko siku watajua

UKURASA 20



# Shoo: Acheni kutesa watu

- **Aonya** mahakama, vyombo vya dola, maaskofu watoa ujumbe mzito Krismasi... *Endelea ukurasa 2 & 3*




"Tusiogope mjadala wa Katiba na hata wale wanaofanya mjadala huo tusiwaone kama maadui, watu wote hawawezi kuwa na mawazo sawa.

**Askofu Dk. Gaula**



"Unakuta vijana wanatembea uchi na wametoka nyumbani. Wazazi na walezi mpo na mnawaona hamuongei, badilikeni.

**Askofu Minde**



"Viongozi wanapokuwa na uchu na madaraka, husababisha mafarakano, chuki, ubaguzi kisha kuvuruga amani ya nchi.

**Askofu Sangu**



"Baadhi ya wanafunzi vyuoni, wamekuwa wakiishi kinyumba... wamekuwa wakistarehe na wakati mwingine kutoa mimba wanazopata.

**Askofu Mkuu Amani**



# Elimu corona yatolewa makanisani, chanjo leo

UKURASA 4

**MICHEZO** | **YANGA : BIASHARA HAWAPONI** UK.24 | **MAONI, KATUNI** UK.6

# Samia atoa zawadi Krismasi wasioona

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

RAIS Samia Suluhu Hassan ametoa zawadi mbalimbali kwa wakazi wa Kituo cha Wasioona cha Watu Wazima Buigiri-Matembe Bora, kilichoko kata ya Buigiri, wilaya ya Chamwino mkoani Dodoma.

Akizungumza kwa niaba ya Rais baada ya kukabidhi zawadi hizo jana, Kaimu Mkurugenzi Huduma za Ikulu, Daniel Mwalusamba, alisema lengo la zawadi hizo ni kushiriki pamoja na makundi maalumu katika kusherehekea Sikukuu ya Krismasi na Mwaka Mpya.

"Zawadi hii ni sehemu ya salamu za Krismasi ambayo imetolewa na mama yetu na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan, katika kuwajali jirani zake na watu wenye mahitaji maalumu," alisema.

Mwalusamba alisema Rais Samia anawatakia heri ya sikukuu watu hao, akisisitiza kuwa wanapaswa kusherehekea kwa amani na utulivu.

Sambamba na hayo, alitumia nafasi hiyo kutoa wito kwa wadau mbalimbali wa maendeleo nchini kuendelea kusaidia wenye mahitaji maalumu katika kipindi hiki cha sikukuuu ikiwa ni ishara ya kuwaenzi, hali itakayowatoa kwenye upweke.

Mwenyekiti wa Kituo hicho, Yared Cheleso, alimshukuru Rais Samia kwa zawadi hizo na kueleza kuwa huo ni upendo unaopaswa kuigwa na wadau wengine huku akimtakia heri ya afya njema na utendaji mwema wa kazi.

Alisema kuwa watu wenye ulemavu wa macho wamekuwa na matumaini na uongozi wake na wapo pamoja katika mapambano dhidi ya ugonjwa wa UVIKO-19 kwa kila hatua.

"Wewe ni mama yetu, tunakuamini, endelea kufanya kazi na sisi tupo nyuma yako katika mapambano haya dhidi ya UVIKO-19, tupo pamoja na tunajitahidi kufuata hatua zote za kujikinga na kuwaelimisha wengine," alisema.



Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, akiwa na mkewe, Mama Mbonimpaye Mpango, wakiwa na waumini wa Kanisa Katoliki la Mtakatifu Paulo wa Msalaba, Jimbo Kuu la Dodoma katika ibada ya ya Krismasi iliyoongozwa na Padri Julius Soteri jana. **PICHA: OFISI YA MAKAMU WA RAIS**

# Dk. Shoo: Acheni kutesa watu

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

MKUU wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Askofu Dk. Frederick Shoo, amewanyooshea kidole mahakimu, vyombo vya dola na majaji, akiwataka wajiepushe kushiriki dhambi ya kutesa wengine kwa kuwa Mungu anaweza kubadilisha furaha kuwa vicheko na wanaofurahi na kushangilia wakawa kwenye vilio.

Askofu Dk. Shoo, ambaye pia ni Mkuu wa Dayosisi ya Kaskazini, alionya hayo jana wakati akitoa salamu zake za Krismasi katika Kanisa Kuu la Usharika wa Moshi Mjini.

"Tuache na tukatae vitendo vya hila vinavyosababisha maumivu kwa wenzetu, vinavyosababisha uchungu kwa wenzetu na familia zao. "Wito wangu kwa walezi, wazazi, vyombo vya dola, mahakimu, majaji, acheni kuwaonea watu.

"Kwa sababu kuwatesa wengine, ndugu zangu tusifikiri kwamba Mungu haoni, tunasema Mungu anaona, tena Mungu anasikia vilio, anaona machozi na huzuni za wale wote wanaonewa.

"Lakini tujue kwanza kwake Mungu wetu kama tulivyoona alivyobadilisha huzuni, upweke, hali ya kuwa na hofu kwa wale wachungaji, kwake sio jambo gumu," alionya.

Askofu Dk. Shoo alisema kwa kuwa Mungu anasikia, kwake sio jambo gumu kubadilisha huzuni ya wale wenye huzuni, wanaolia sasa kuwa furaha.

Dk. Shoo aliendda mbali zaidi akisema, kwake sio jambo gumu kubadilisha furaha na vicheko vya wanaofurahi na kushangilia kuwa vilio, kwa kuwa yuko Mungu aliye hai.

"Utendapo, ufanyapo, ujue yuko Mungu anayeona. Hivyo basi, tujiepushe na hilo maana Mungu mwenye haki hataacha kulipa kwa wakati wake. Tujiepushe na hayo ili nchi yetu ibarikiwe, familia zetu zibarikiwe na sisi tubarikiwe.

"Kuna mambo yanaendelea katika nchi yetu. Wako watu wanaosababisha wenzao wakose amani. Wanawasababishia maumivu na uchungu moyoni, maumivu ambayo yanagusa hata familia za hao wenzetu.

"Na wanafanya hivyo kwa sababu tu wanayo nguvu, wana nafasi, wana mamlaka," Askofu Dk. Shoo alisema.

# Askofu Gaula aibua mjadala wa Katiba

**Na Waandishi Wetu**

KANISA la Anglikana Dayosisi ya Kondoa katika ujumbe wake wa Krismasi limetaja mambo 10, ikiwamo kutoa ushauri wa kutowaona kama maadui wale wanaoendelea na mjadala wa kudai Katiba Mpya.

Akisoma ujumbe wa Krismasi kwa niaba ya kanisa, Askofu wa Kanisa la Anglikana Dayosisi ya Kondoa, Dk. Given Gaula, alisema hakuna haja ya kuogopa kufanyika kwa mjadala wa Katiba kwa sababu kila mtu ana uhuru wa kutoa mawazo yake.

"Tusiogope mjadala wa Katiba, na hata wale wanaofanya mjadala huo tusiwaone kama maadui kwa sababu kila mtu ana uhuru wa kutoa mawazo yake na watu wote hawawezi kuwa na mawazo sawa, na kila jambo lina wakati wake," alisema.

Askofu Gaula alitaja jambo la pili ni kuiomba serikali kuhakikisha inatenda haki kwa kila mtu ili kuendelea kulinda amani iliyopo na kwamba hilo ndilo litakuwa msingi wa kuendelea kulinda amani iliyopo.

Jambo la tatu ni kuipongeza serikali kwa kuweka uwazi katika kushughulikia suala la virusi vya corona ikiwamo kuagiza chanjo.

Alisema wanampongeza Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuonyesha ukomavu wa kisiasa na kurejesha furaha iliyokuwa imepotea kwa Watanzania, kuonyesha huruma na upendo.

Askofu Gaula alisema jambo lao la tano ni kuiomba serikali iendelee kutilia mkazo katika kupiga vita ubaguzi wa aina yoyote na kuhakikisha inashughulikia kero za sekta zote kwa usawa bila kubagua, akionya masuala ya ukabila na udini.

"Kwa mfano kama tunavyoona serikali ikishughulikia sekta ya afya kwa kuweka mazingira mazuri ikiwamo kujenga vituo vya afya, tunaomba pia na katika sekta ya elimu isibague, tumeona sasa hivi inajenga vyumba vya madarasa kwa wingi lakini ukienda huko vijijini walimu hakuna," alisema Askofu Gaula.

Alilitaja jambo la sita ni kupongeza jitihada zinazofanyika sasa katika kupambana na vitendo vya unyanyasaji wa kijinsia.

Pia kanisa hilo lilipongeza utaratibu unaofanywa na serikali katika uteuzi wa makundi mbalimbali ya viongozi wake, lakini akawa na tahadhari kwamba kufanyike uchunguzi wa kutosha na kujiridhisha katika uteuzi wa kundi la vijana kwa kuwa ndilo lililo kwenye hatari kubwa ya vitendo vya rushwa.

Jambo la nane ni serikali itumie kwa kiwango kikubwa wazee kwenye mambo mbalimbali yanayohitaji ushauri na pia kutolisahau wala kulipuuza kundi hilo katika mambo mengine.

Alisema kuwa jambo lao la tisa ni kuiomba serikali kuweka mkazo kwenye udhibiti wa uharibifu wa mazingira unaosababisha ukame, wakishauri kuwekwa mazingira ya matumizi ya mkaa yawe ghali na kupunguza gharama za gesi.

Askofu huyo alitaja jambo la 10 ni wanawake wanaoaminiwa na kupewa nafasi za uongozi, waonyeshe mfano kwa kuchapa kazi kama ilivyo kwa Rais Samia, huku wakitenda haki kwa watu wote na kuonyesha kwamba walistahili nafasi hizo.

**MALEZI YA WATOTO**

Katika Parokia ya Kristu Mfalme Jimbo la Moshi, Mhashamu Askofu Ludovick Minde, aliwataka waumini Jimbo Katoliki la Moshi kuacha tabia za kuwaogopa watoto na badala yake kuwaonya kulingana na taratibu na sheria za nchi ikiwa watawashinda.

Alisema vijana kwa sasa wamekosa maadili na kujiingiza kwenye makundi yasiyofaa kutokana na wazazi na walezi kuwafumbia macho watoto wanapopungukiwa maarifa.

"Acheni kuwaogopa na kuwadekeza hao watoto, mnatengeneza mzigo mzito kwa nchi, wakemeeni, waonyeni. Unakuta vijana wanatembea uchi na wametoka nyumbani wazazi na walezi mpo na mnawaona hamwongei, badilikeni!" aliasa.

Jijini Dar es Salaam, Askofu Mkuu wa Jimbo Kuu Katoliki la Dar es Salaam, Mhashamu Yuda Thaddeus Ruwa`ichi, aliwataka waumini kutojihusisha na mambo maovu ili toba zao zipokewe na wafanikiwe katika yale yote wanayoyaomba.

■**Imeandikwa na Elizabeth Zaya, Mary Mosha (MOSHI) na Maulid Mmbaga (DAR)**

# Nasaha za Maaskofu Krismasi

## ■Bandari ya Bagamoyo yaguswa

WAUMINI wa madhehebu ya Kikristo nchini wameungana na waumini wengine wa madhehebu hayo duniani kuadhimisha Sikukuu ya Krismasi, huku maaskofu wakitoa nasaha kwa jamii na viongozi wa kiserikali.

Katika kusherehekea sikukuu hiyo, miongoni mwa mambo yaliyozungumzwa na viongozi hao wa kiroho kwenye mahubiri yao kuanzia kwenye mkesha wa Krismasi usiku wa kuamkia jana na jana asubuhi wakati wa ibada ya Krismasi, ni tabia ya uchu wa madaraka kwa baadhi ya viongozi.

Vilevile, ujenzi wa Bandari ya Bagamoyo na utulivu uliotokana na kuundwa kwa Serikali ya Umoja wa Kitaifa Zanzibar uliguswa na viongozi hao kwenye mahubiri yao.



Waumini wa Kikristo wa Kanisa la Mtakatifu Albano jijini Dar es Salaam wakifuatilia mahubiri ya Krismasi jana. PICHA: JUMANNE JUMA

**SANGU NA MADARAKA**

Mjini Shinyanga, Askofu wa Kanisa la Katoliki Jimbo la Shinyanga, Mhashamu Liberatus Sangu, katika misa ya mkesha wa Sikukuu ya Krismasi katika Kanisa la Katoliki la Mama Mwenye Huruma Parokia ya Ngokolo, alikemea viongozi kuwa na uchu wa madaraka.

Alisema viongozi wanapokuwa na uchu na madaraka, husababisha mafarakano, chuki, ubaguzi na kisha kuvuruga amani ya nchi.

"Ndugu zangu vita vinavyoendelea Congo na mataifa mengine, ni sababu ya viongozi kuwa na uchu wa madaraka, ninawaomba viongozi wetu nchini wasiwe na uchu wa madaraka, ili kudumisha amani ya nchi," alisema Askofu Sangu.

"Ninaomba pia viongozi na wananchi wawe na hofu ya Mungu, sababu chimbuko la amani ni Yesu pamoja na kuishi kwa upendo na kuacha kuendekeza masuala ya ukatili wa kijinsia na mauaji ya watu wasiokuwa na hatia," aliongeza.

Askofu Sangu pia aliwataka Watanzania kila mmoja kwa imani yake kuombea hali ya hewa ili mvua inyeshe kwa wingi na kusitokee baa la njaa baadaye, ili wananchi walime mazao na kupata chakula.

Pia aliwataka wananchi na waumini wa kanisa hilo katika kusherehekea Sikukuu ya Krismasi na Mwaka Mpya wawe majumbani mwao na siyo kwenda kufanya mambo ya anasa, huku akitamani kwenye sherehe hizo mvua inyeshe kutwa nzima ili "watu wasitoke out" (kufanya starehe).

Kiongozi huyo wa kiroho pia alilipongeza Jeshi la Polisi kwa kuzuia disko toto, ambayo imekuwa ikihatarisha usalama wa watoto na kuwataka wazazi wazuie watoto wao kuzurura ovyo mitaani, bali washinde nao majumbuni na kusheherekea sikukuu pamoja.

Mkuu wa Wilaya ya Shinyanga, Jasinta Mboneko, akitoa salamu za serikali, aliwaomba viongozi wa dini kuendelea kuombea amani ya nchi pamoja na mvua, huku akiwahakikishia wananchi katika sherehe za mwisho wa mwaka wataendelea kudumisha amani na utulivu.

Mboneko alikazia pia kauli ya Kamanda wa Jeshi la Polisi mkoani Shinyanga, George Kyando, kuwa kwa wale walevi na waliojipanga kufanya fujo katika sikukuu hizo, serikali itawashughulikia na watakula sikukuu wakiwa mahabusu.

**MSIMBE AONYA UKATILI**

Mjini Morogoro, Askofu wa Jimbo Katoliki Morogoro, Razalus Msimbe, aliitaka jamii kumtegemea Mungu katika kukabiliana na vitendo vya ukatili wa kijinsia vinavyotokea kwa wingi kwa sasa nchini.

Alisema vitendo vya ukatili wa kijinsia ikiwamo mauaji na kutupa watoto vinavyofanywa na baadhi ya jamii, vinazidi kuongezeka siku kwa siku na huenda jamii imejisahau kumwomba Mungu aiepushe na janga hilo.

**SHAO NA UTULIVU ZANZIBAR**

Visiwani Zanzibar, Askofu wa Kanisa Katoliki Minara Miwili Zanzibar, Agostino Shao, alisema Serikali ya Umoja wa Kitaifa imeleta utulivu na amani visiwani humo.

Alisema serikali hiyo imejenga fursa ya kuzungumzia kasoro zilizopo, akibainisha kuwa kutofautiana kimawazo au kisera si uadui, bali ni fursa na hamasa ya namna tofauti ya kuleta maendeleo.

"Tunampongeza Rais wetu, Dk. (Hussein) Mwinyi kwa njia ya mazungumzo amerudisha Serikali ya Umoja wa Kitaifa," alisema na kubainisha kuwa ujumbe wa Krismasi mwaka huu ni kuwa wamoja, kujenga pamoja maendeleo ya nchi lakini wananchi wabaki na tofauti zao.

Askofu Shao alitoa angalizo kwa serikali katika kujenga uchumi wa bluu na viwanda, akiitakia kujiweka tayari kuandaa vijana kitaaluma ili kupata ajira.

**VIJANA NA UZINZI**

Jijini Mwanza wakati wa mkesha wa Krismasi Askofu Mkuu wa Kanisa la Living Water, Onesmo Ndege, aliwataka vijana kutambua siku ya kuzaliwa kwa Yesu Kristo kuwa ni muhimu kwa kila mtu, hivyo waachane na dhambi na wapendane.

Alisema vijana wapo katika hatari ya kukumbana na mambo mengi, akisisitiza kuwa wakitaka kuishi maisha ya furaha na amani, wamfuate Yesu kwa kuwa ndiye aijuaye kesho ya kila mtu na amezaliwa kwa ajili ya kuwafundisha njia ipasayo ya kumfuata Mungu.

"Nikiangalia hapa asilimia kubwa ni vijana, achaneni na uzinzi, tabia mbaya na makundi yasiyo sahihi muwaheshimu wazazi wenu, mpendane. Hiyo itakuwa faida yenu ya baadaye kwani kazi ya roho mtakatifu ni ubunifu, muishi ndani ya Kristo ili kuwa na amani na kila dhambi zinakufa ukiwa naye," aliasa.

**SENSA, BANDARI BAGAMOYO**

Jijini Arusha Askofu Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) Dayosisi ya Kaskazini Kati, Dk. Solomon Massangwa, aliwataka wakristo na Watanzania kushiriki kikamilifu na kujitokeza kuhesabiwa wakati wa Sensa ya Watu na Makazi kwa kuwa ni muhimu katika mipango ya maendeleo ya taifa. Serikali imepanga kufanya sensa hiyo mwezi Agosti mwakani.

Dk. Massangwa alisema kuna umuhimu wa hesabu katika mpangilio wa maendeleo ya binadamu na ukombozi.

"Kwa kufanya hesabu kuna siri kubwa iliyojificha hapo, kutoka Nazareth mpaka Bethlehem kwenda kuhesabiwa, kuandikwa na kuwekwa kwenye orodha iliwagharimu Mariamu na Yusuph siku tano wakitembea kwa mguu na ni kama kilomita 144.8.

"Tunaona hapa kuna siri kwa kuwa familia ya Mungu ikitii amri iliyowekwa, lakini siyo kutii tu familia hiyo iliona umuhimu wa hesabu katika mpangilio wa maendeleo ya binadamu na ukombozi kwa kuwa walitembea siku zote kwa umbali wa maili 17 mpaka 20 huku wakipigwa na jua, baridi na njaa ili kutii amri iliyowekwa.

"Mwakani Mungu akipenda Tanzania, tutakwenda kufanya Sensa ya Watu na Makazi. Ndugu zangu kuna siri ndani ya takwimu katika ukombozi wa binadamu, usipofahamu idadi ya watu katika familia yako, huwezi kujua utawalisha kitu gani," alifafanua.

Katika hatua nyingine, Askofu Dk. Massangwa alisema ujenzi wa Bandari ya Bagamoyo unaweza kufanywa na Watanzania wenyewe wakiamua kuchangia ujenzi huo badala ya kuwategemea wawekezaji.

"Nilikuwa naangalia hesabu za gharama za ujenzi wa Bandari ya Bagamoyo, thamani ya ujenzi ni wa dola za kimarekani bilioni 18 , sawa na Sh. trilioni 24.

"Watanzania tupo milioni 57, tukipunguza tukabaki milioni 20, tukagawanya kwa trilioni 24, kila mmoja angechangia Sh. milioni 1.4 na mwisho wa siku tunaikabidhi serikali mradi huo.

"Kama Wakristo wa KKKT wakiamua kujenga bandari hiyo, wenyewe tupo kati ya milioni saba mpaka nane, hivyo kila mkristo atachangia milioni 4.8. Hakuna haja ya kuogopa hizo hesabu, bali ni kuangalia nguvu iliyokuwapo ndani ya hesabu na siku zote ukitaka kusonga mbele, usiogope vihatarishi na wakristo huwa hawashindwi na jambo lolote," alisema Dk. Massangwa.

**KINYUNYU NA WANASIASA**

Mkoani Dodoma Askofu wa KKKT Dayosisi ya Dodoma, Amon Kinyunyu, aliwataka wanasiasa kuendelea kudumisha amani ili taifa lizidi kuwa na ustawi.

"Hakuna mamalaka iliyopo isiyotokana na Mungu, hata viongozi wetu wa nchi waliopo wamewekwa na yeye Mungu. Kwa hiyo tunatakiwa kuwatii na kuwaombea katika nafasi zao ili watuongoze kwa amani," alisema,.

Aliwataka viongozi wa kisiasa kuheshimiana pamoja na kujali amani na mustakabali wa taifa ili watu wakue kiuchumi.

Kiongozi huyo pia alihimiza Watanzania kushiriki katika Sensa ya Watu na Makazi mwakani, akibainsha kuwa utaratibu huo upo kwa miaka mingi ya nyuma na ndio maana Yesu Kristo alizaliwa wakati wazazi wake walipokwenda kuhesabiwa huko kwao.

Akofu Mkuu wa Jimbo Kuu Katoliki la Dodoma, Beatus Kinyaiya, alitoa wito kwa Watanzania kuendelea kuwaombea viongozi wa serikali ili waendelee kuwaongoza wananchi kadri ya mapenzi ya Mungu.

Makamu Askofu Mkuu wa Kanisa la Anglikana Tanzania, Dk. Dickson Chilongani, aliwataka viongozi wa ngazi mbalimbali kushuka chini kwa wananchi kujua matatizo yao badala ya kutoa maagizo wakiwa ofisini.

Alisema kuwa viongozi wengi wamekuwa na tabia ya kukaa ofisini na kutoa maagizo badala ya kushuka kwa watu wanaowaongoza na kujua matatizo yao.

***Imeandikwa na Marco Maduhu (SHINYANGA), Christina Haule (MOROGORO), Rahma Suleiman (ZANZIBAR), Neema Emmanuel (MWANZA), Allan Isack (ARUSHA), Ibrahim Joseph, Paul Mabeja, Renatha Msungu na Peter Mkwavila (DODOMA)**

# Waumini wapewa elimu ya chanjo UVIKO-19

**Na Mary Geofrey, SINGIDA**

WATAALAMU wa Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) wametembelea makanisa mbalimbali wilayani Singida mkoani Singida na kutoa elimu ya chanjo ya UVIKO-19 na kuwahamasisha waumini hao kuchanja kwa hiari.

Timu ya wataalamu hao jana ilitembelea Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) Dayosisi ya Kati, Usharika wa Emmanuel na Nazareth na Kanisa Katoliki Singida, Assembles of God na FPCT Singida Mjini na kuzungumza na waumini waliokuwa katika ibada ya kusherekea Sikukuu ya Krismasi.

Mtaalamu wa Ufuatilia na Udhibiti wa Magonjwa kutoka Wizara ya Afya, Dk. Baraka Nzobo, akizungumza na waumini wa Kanisa la KKKT, Usharika wa Emmanuel, aliwataka kuendelea kujikinga na kuchukua tahadhari dhidi ya UVIKO-19.

Aliwataka waumini hao kuachana na dhana potofu kuhusu chanjo kwa sababu wapo waliochanja na wanaendelea na shughuli zao za kila siku na hakuna madhara yoyote.

Aliwataka waumini watakaokuwa tayari, kujitokeza katika ibada ya leo Jumapili kwa ajili ya kupata chanjo ya UVIKO-19 ili kujikinga na hatari ya maambukizo ya ugonjwa huo.

Alisema wapo wataalamu wanaendelea kutembea nyumba kwa nyumba na mtaa kwa mtaa katika mkoa huo, ili kutoa huduma hiyo, hivyo wasipoteze fursa ya kuchanjwa wakiwa nyumbani.

Akiwa katika Kanisa la FPCT, aliwataka waumini hao kuendelea kuchukua tahadhari kwa kuvaa barakoa, kukaa kwa kupeana nafasi na kupata chanjo ya UVIKO-19 ili kuwa salama zaidi.

Alisema serikali inafanya jitihada za kuwakinga wananchi wake, wakiwamo waumini wa makanisa mbalimbali ambako wanawatembelea wakiwa ibadani ili kuwapa uelewa kuhusu umuhimu wa chanjo.

Askofu wa Kanisa la FPCT mjini Singida, Dk. Paulo Njoghomi, aliwataka waumini wao kuacha kupuuza taarifa za wataalamu wa afya kwa sababu ugonjwa huo upo, umeua watu wengi na kuvuruga uchumi.

Aliwataka kujitokeza kupata chanjo itakayotolewa leo kanisani huko na wataalamu wa afya ili kuwa na uhakika na maisha yao.

Mkoa wa Singida ni moja ya mikoa inayotekeleza Kampeni ya Kuhamasisha Utoaji wa Chanjo ya UVIKO-19 katika Mpango Shirikishi na Harakishi Awamu ya Pili, unaotekelezwa nchi nzima na Wizara ya Afya kupitia Kitengo cha Elimu kwa Umma.

# WB kujenga kiwanda kuzalisha dawa nchini

**Na Ismail Makongo**

WAZIRI wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Dorothy Gwajima, amemhakikishia Kaimu Mkurugenzi wa Benki ya Dunia (WB) na Mkurugenzi wa Masuala ya Maendeleo ya Watu kwa Nchi za Tanzania, Zambia, Malawi na Zimbabwe kuwa Tanzania iko tayari kushirikiana na benki hiyo katika kutekeleza afua ya chanjo, wakati dunia inapokabiliwa na ugonjwa wa UVIKO-19.

Dk. Dorothy alitoa kauli hiyo juzi katika kikao cha majadiliano kati yake na mwakilishi wa WB kilichofanyika Ofisi za Wizara ya Afya jijini Dar es Salaam.

Waziri huyo alisema Wizara ya Afya imeanzisha mkakati wa kushirikisha vyombo vya habari, viongozi wa dini, wanasiasa na watu maarufu kwa lengo la kuwafikia watu wengi zaidi ili wapatiwe chanjo ya UVIKO-19 wakiwa kwenye maeneo yao.

"Kwa sasa tupo katika awamu ya pili ya Mpango Shirikishi na Harakishi kwenye Masuala ya Kupambana na UVIKO-19, ambao tuliuzindua mkoani Arusha, kaskazini mwa nchi yetu Desemba 22 mwaka huu.

"Na maelekezo yamekwenda kwa wakuu wa mikoa, wakuu wa wilaya na wakurugenzi wa mamlaka za serikali za mitaa, ambao kwa pamoja wanashirikiana kwa karibu zaidi na wananchi katika kutoa elimu ya chanjo kwa kuwatumia watoa huduma kwenye ngazi ya msingi kisha kupatiwa chanjo," alisema.

**KIWANDA CHA DAWA**

Kaimu Mkurugenzi wa WB na Masuala ya Maendeleo ya Watu katika nchi za Tanzania, Zambia, Malawi na Zimbabwe, Inaam Ui-Haq, alisema benki hiyo imeonyesha utayari kwa Tanzania katika uwekezaji wa kiwanda cha kuzalisha dawa za binadamu na kusaidia masuala ya chanjo ya UVIKO-19, Mama na Mtoto, ili wananchi wapate dawa kwa wakati pindi wanapofuata huduma katika vituo vya afya.

"Benki ya Dunia tupo tayari kusaidia Tanzania, lakini vyema likapatikana andiko juu ya UVIKO-19 pamoja na masuala ya Mama na Mtoto, kwa maeneo ambayo kama nchi inaona ni muhimu kuyaangazia kwa upekee," alisema Ui-Haq.



Viongozi wa Kanisa la Glory Temple la mjini Tanga wakitoa msaada kwa makundi mbalimbali yenye mahitaji maalumu kanisani ikiwa ni sehemu ya kusherehekea Sikukuu ya Krismasi jana. **PICHA: BONIFACE GIDEON**

# Ndumbaro aona fursa ajira kutoka kwa wawekezaji

**Na Amon Mtega,** SONGEA

MBUNGE wa Songea Mjini, Dk. Damas Ndumbaro, amewataka wakazi wa jimbo hilo kuzitumia vyema fursa mbalimbali zikiwamo za ajira zitokanazo na wawekezaji walioonyesha nia ya kuwekeza kwenye jimbo hilo.

Dk. Ndumbaro ambaye pia ni Waziri wa Maliasili na Utalii, alitoa wito huo juzi alipozindua maeneo ya uwekezaji wa viwanda yaliyopo kata ya Lilambo, Manispaa ya Songea mkoani humo.

Uzinduzi huo ulikwenda sambamba na kuvitambua vikundi 11 vya ujasiriamali ambavyo vimepatiwa mkopo wa Sh. milioni 465 kwa makundi ya fani mbalimbali ikiwamo ya ushonaji nguo.

Katika uzinduzi huo uliohudhuriwa na viongozi mbalimbali wa chama na serikali, akiwamo Mwenyekiti wa Wafanyabiashara wa China Afrika, Xian Qsag, maarufu Komba, Dk. Ndumbaro alisema kwamba kama wakazi wa jimbo hilo wakitumia ipasavyo fursa zinazoletwa na wawekezaji, manispaa hiyo itabadilika kwa kasi na itapewa hadhi ya jiji.

Mbunge huyo alisema kuwa eneo hilo walilotengewa wawekezaji wa viwanda, litatumika ipasavyo ikiwamo kuweka miundombinu stahiki ili wajasiriamali ambao wengi wao wanapatiwa mikopo ya asilimia 10 ya mapato ya ndani, wanufaike zaidi.

Mbunge huyo wakati akikabidhi hundi za malipo kwenye vikundi hivyo, fedha zikiwekwa kwenye akaunti za benki, alisema kwa sasa ni wakati mzuri wa kufanya kazi kwa kujituma zaidi.

Alitumia nafasi hiyo kueleza mambo kadhaa hasa ya miradi iliyofanywa na jimbo hilo katika sekta mbalimbali kama afya, elimu na barabara pamoja na utekelezaji wa miradi miwili ya ujenzi wa dampo na soko.

Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Manispaa ya Songea, Beno Philipo, alisema vikundi vilivyopatiwa mikopo hiyo ni vya vijana, wanawake na watu wenye ulemavu, akibainisha kuwa watu wenye ulemavu wamekuwa warejeshaji wazuri wa mikopo hiyo.

Philipo alisema halmashauri itaendelea kuvijengea uwezo vikundi kwa kutoa mafunzo na vifaa, akionya kuwa baadhi yao wamekuwa wakigawana fedha za mkopo badala ya kufanya kilichokusudiwa wakati wa maombi ya mkopo huo.

Mkuu wa Wilaya ya Songea, Pololet Mgema, alimtaka Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo pamoja na timu yake kuhakikisha wanakusanya fedha za madeni zilizopo kwenye vikundi vilivyokopa ili kutoa fursa na vikundi vingine kukopeshwa.

Diwani wa Lilambo, Yobo Mapunda, aliwaomba watalaamu wa mipango miji kutoka manispaa kwenda kupima maeneo hayo haraka ili kutoa fursa ya wawekezaji kujenga.

Mwenyekiti wa wafanyabiashara wa China Afrika, Xian Qsag, alisema Songea ni kati ya maeneo mazuri barani Afrika kwa uwekezaji huku akiwaomba wakazi wa jimbo hilo kutambua jitihada zinazofanywa na mbunge wao kuwapelekea maendeleo wananchi.

Mmoja wa waliopatiwa mikopo hiyo, Josephina Mhagama, Mwenyekiti wa Kikundi cha Ushonaji wa Nguo kilichoko Mjimwema, aliipongeza serikali kwa kukitambua kikundi hicho kisha kupatiwa mkopo.

HABARI KITAIFA

# Wanawake wapewa mbinu kupata zabuni

**Na Mwandishi Wetu**

KATIBU Mtendaji wa Baraza la Uwezeshaji wa Wananchi Kiuchumi (NEEC), amewahamasisha wanawake kuhakikisha wanatumia maendeleo ya teknolojia kujiunga na Mfumo wa Ununuzi kwa Njia ya Mtandao (TANePS) ili wapate kushiriki fursa za zabuni za umma pamoja na biashara zingine.

Beng'i Issa alitoa rai hiyo juzi alipofungua mafunzo ya Sheria ya Ununuzi wa Umma na jinsi ya kutumia TANePS yaliyoandaliwa na Mamlaka ya Kudhibiti Ununuzi wa Umma (PPRA) kwa ajili ya wanawake wa Mkoa wa Iringa na mikoa ya jirani.

Alisema kuwa serikali kupitia PPRA imeanzisha TANePS na kutoa maelekezo kuwa michakato ya zabuni zote za umma itafanyika kupitia mfumo huo na wanawake ambao wamepewa fursa ya upendeleo kama kundi maalumu kwenye Sheria ya Ununuzi wa Umma, wanapaswa kuhakikisha wanafahamu jinsi ya kujisajili na kutumia mfumo huo ili wapate fursa hizo.

"Tumieni sana simu mlizonazo, ambazo zina uwezo karibu sawa na kompyuta kukuza biashara zenu na kujiunga na fursa za zabuni kupitia TANePS. Mafunzo mtakayoyapata hapa kuhusu TANePS na Sheria ya Ununuzi wa Umma mkayatumie ipasavyo na kuwahamasisha wanawake wengine kutumia teknolojia kupata fursa za zabuni za umma ili wajikwamue kiuchumi," alisema.

Katibu Mtendaji huyo alitoa wito kwa wanawake hao kuhakikisha wanajisajili kwenye vikundi na kupata sifa ya kuorodheshwa kama kundi maalum la wanawake, ili wapate fursa ya nafasi ya upendeleo wa makundi maalum inayotolewa na Sheria ya Ununuzi wa Umma.

Alisema sheria hiyo inazitaka taasisi serikali kutenga asilimia 30 ya bajeti yake ya ununuzi kwa ajili ya makundi maalumu ambayo ni wanawake, wazee, vijana na watu wenye ulemavu.

Awali, Ofisa Mtendaji Mkuu wa PPRA, Dk. Irene Isaka, alisema jumla ya makundi 40 tu ndio yaliyokidhi vigezo vya usajili kama kundi maalumu na kuorodheshwa na PPRA.

Alisema kuwa ingawa idadi hiyo ya ya kundi la wanawake ni kubwa kulinganisha na makundi mengine ya wazee, vijana na watu wenye ulemavu, bado ni ndogo kwa kuzingatia kuwa asilimia 54 ya wajasiriamali nchini ni wanawake.

Dk. Isaka pia alitoa rai kwa washiriki kuwa waamini na waadilifu wanaposhiriki michakato ya zabuni za umma kwa kuwa uadilifu ndio nguzo kuu ya ununuzi wa umma ili kupata thamani halisi ya fedha.

Akizungumza kwa niaba ya washiriki wa mafunzo hayo, Mwenyekiti wa Chama cha Wafanyabiashara Wanawake Tanzania (TWCC) Mkoa Iringa, Flora Sumaye, aliishukuru PPRA na serikali kwa ujumla kwa kuwajengea uwezo wanawake wa mkoa huo ili wazipate fursa za zabuni za umma.

Mafunzo hayo kwa wanawake wajasiriamali yaliyogharamiwa kwa asilimia 100 na serikali kupitia PPRA, chini ya ufadhili wa Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB), yamefanyika katika mikoa mitano ambayo ni Kilimanjaro, Morogoro, Mbeya, Dar es Salaam na Iringa.




Watoto wa Kituo cha Watoto yatima cha New Hope wakiwa katika picha ya pamoja na wafanyakazi wa Kampuni ya Sukari Kilombero (KSCL), Unitrans, viongozi wa kijiji na kata katika hafla iliyoandaliwa na Unitrans kwa kushirikiana na KSCL kama sehemu ya mikakati ya kusaidia jamii. Kampuni hizo zilikabidhi misaada mbalimbali na choo kilichojengwa na KSCL chenye thamani ya takriban milioni 11. Hafla hiyo ilifanyika Desemba 22, 2021, katika kijiji cha Kitete, Kilombero.

# Ajali ya lori yaua watu wanne

**Na Lilian Lugakingira,** BUKOBA

WATU wanne wamepoteza maisha baada ya gari la mizigo aina ya Scania lenye namba za usajili T 654 DRW walilokuwa wakisafiria, kuacha njia na kupinduka katika mteremko wa Kishoju, kata ya Kihanga wilayani Karagwe mkoani Kagera.

Kamanda wa Polisi mkoani Kagera, Awadhi Haji, alisema gari hilo lenye tela lenye namba za usajili T 638 ADD, wakati linapata ajali Desemba 23 mwaka huu saa tatu asubuhi, lilikuwa limepakia shehena ya magogo na lilikuwa likitokea wilayani Karagwe kwenda mkoani Shinyanga.

Aliwataja waliopoteza maisha kuwa ni Said Twalibu (27), mkazi wa Igombero, Mkinga mkoani Tanga aliyekuwa dereva wa gari hilo, Mohamed Seif (31), mkazi wa Mkinga Emmanuel Salu, mfanyabiashara wa Kahama na Yasin Gowa, mkazi wa Tarime mkoani Mara.

"Eneo la tukio barabara ina mteremko mkali na kona kali, uchunguzi wa awali unaonyesha chanzo cha ajali hiyo ni uzembe wa dereva ambaye naye sasa ni marehemu, alishindwa kuchukua tahadhari kwenye mteremko huo na mvua ilikuwa inanyesha lakini pia kulikuwa na ukungu mwingi," alisema.

Kwa mujibu wa Kamanda Haji, miili ya watu hao imehifadhiwa kwenye Hospitali ya Nyakahanga iliyoko wilayani Karagwe kwa ajili ya uchunguzi zaidi.

Kufuatia tukio hilo, jeshi la polisi limewaonya madereva kuacha uzembe wawapo barabarani hasa wakati mvua inaponyesha na kuwataka kuzingatia sheria za usalama barabarani ili kuepusha kutokea ajali ambazo husababisha vifo, ulemavu na uharibifu wa mali.

# Madereva wanaosababisha ajali kizembe kitanzini

**Na Gideon Msakanosya,** SONGEA

MKUU wa Kikosi cha Usalama Barabarani mkoani Ruvuma, Mrakibu wa Polisi, Salum Morimori, amewataka madereva wa vyombo vya moto kuzingatia kanuni za udereva ili kuepusha ajali ambazo hutokea kutokana na uzembe.

Alitoa angalizo hilo jana alipofanya ukaguzi wa kushtukiza kwenye vituo vya mabasi vya shule ya Tanga na Mfaranyaki kisha kuzungumza na madereva wa mabasi hayo na kuwaonya kuhusu hatari ya kutokea kwa ajali kipindi hiki cha sikukuu za mwishoni wa mwaka kutokana na wingi wa magari barabarani.

Morimori alisema ukaguzi huo umejumuisha mabasi ya abiria yanayofanya safari ndefu ndani ya mkoa na nje ya mkoa pamoja na daladala zinazofanya kazi katika Halmashauri ya Manispaa ya Songea.

Alisema ukaguzi wao ulijumuisha jumla ya magari 43 kati yake, 12 yamebainika kuwa ni mabovu na yameondolewa barabarani hadi yatakapofanyiwa matengenezo na wamiliki wa magari hayo na kwamba madereva watatu wa daladala zilizokutwa kuwa ni mbovu wakati ukaguzi ukiwa unaendelea kwenye kituo cha daladala Mfaranyaki, walikimbia na kutokomea kusikojulikana.

Alifafanua kuwa katika ukaguzi huo dosari zilizobainika ni ubovu wa taa, ubovu wa viti, usukani wa magari kutokuwa na nguvu na tatizo la kutokuwa na breki za uhakika, jambo ambalo ni hatari kwa abiria.

Alisema dereva wawili wanashikiliwa na polisi kwa tuhuma mbalimbali, mmoja wao akibainika kuwa hana sifa za kufanya kazi hiyo na mwingine kukutwa akiwa amelewa pombe.

Morimori alisema ukaguzi huo utakuwa endelevu na si kwa ajili ya kipindi hiki cha sikukuu, hivyo akawataka madereva kuhakikisha wanazingatia sheria za usalama barabarani.

Ofisa Mfawidhi wa Mamlaka ya Usafirishaji wa Nchikavu (LATRA) mkoani Ruvuma, Sebastian Lohay, alisema kuwa ofisi yake itaendelea kusimamia taritibu zote za usafirishaji, ikiwamo kuwachukulia hatua wanaokatisha ruti walizopangiwa.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Aliyosema IGP yafanyiwe kazi polisi kujirekebisha

**KWA** muda mrefu, Jeshi la Polisi limekuwa likilalamikiwa na wananchi juu ya mambo ambayo baadhi ya askari wake wanayafanya kinyume cha taratibu na sheria zinazoliongoza ikiwamo utekelezaji wa jukumu lake kuu la kulinda usalama wa raia na mali zao.

Licha ya kushindwa kutekeleza mambo hayo pia baadhi ya askari wamekuwa wakidaiwa kunyanyasa raia, kutumia nguvu kupita kiasi dhidi ya watu wanaowakamata kwa tuhuma mbalimbali na pengine kuwapiga hata kuwasababishia ulemavu wa kudumu kwa kile wanachodai kuwa wanafanya hivyo ili watuhumiwa watoe ushirikiano wa kueleza wanayoyataka wakati wa kutafuta taarifa kuhusu uhalifu unaodaiwa kufanywa na watu hao.

Mambo mengine wanayolalamikiwa askari hao ni kugeuza fursa matatizo ya wananchi pale wanapokwenda kuripoti upotevu wa mali zao kama vile simu. Imedaiwa kuwa wananchi wanaporipoti kupotelewa na simu, baadhi ya askari huwataka kutoa kiasi cha fedha kuanzisha Sh. 50,000. Hata watu wanapopoteza mali huingia gharama kwa kuwapa fedha polisi jambo ambalo kwa mazingira ya waziwazi ni rushwa.

Sambamba na hayo kumekuwa na taarifa za kuwapo kwa vifo vya raia wakiwa mikononi mwa polisi na baadhi ya askari hao kutoa lugha zisizo na staha. Rushwa pia kwa askari wa usalama barabarani na wale wa doria, maarufu kama Tigo, imekuwa gumzo. Mambo hayo kwa kiasi kikubwa yamelitia doa jeshi hilo na hata wananchi kukosa imani nalo.

Mambo hayo hata Rais Samia Suluhu Hassan ameyatamka bayana katika mikutano miwili ya maofisa wakuu na waandamizi wa polisi huku akiweka bayana kwamba wanatakiwa kujirekebisha na kurejea kwenye mstari.

Kutokana na malalamiko kutoka kwa wananchi pamoja na Rais kukemea hadharani, hatimaye Mkuu wa Jeshi hilo, Inspekta Jenerali (IGP) Simon Siro,juzi aliibuka na kutoa maagizo tisa ili kurejesha niidhamu na kuongeza ufanisi katika utendaji wa chombo hicho adhimu kwa usalama wa wananchi.

Akifunga mafunzo ya uongozi Siha mkoani Kilimanjaro, Sirro aliweka wazi kuwa askari hawana budi kuacha lugha zisizo na staha kwa wateja, kuacha kujihusisha na vitendo vya rushwa na kupoteza ushahidi , hivyo kusababisha wananchi kukosa haki.


Pia alisema askari wanapaswa kuwasikiliza wananchi badala ya kutumia mabavu bila sababu na kwa wale wa usalama barabarani, kuacha kuwatoza faini na kutengeneza mazingira ya rushwa dhidi ya watu wanaofanya makosa badala yake watoe onyo.

Bila kuuma maneno, IGP Sirro pia alisema kuna ugonjwa mwingine umezuka ndani ya jeshi hilo kwa wapelelezi kuwabambikizia kesi wananchi kutokana na kupokea rushwa jambo linalosababisha watu wenye hatia kuachiwa huru na wasio na hatia kuumizwa. Alibainisha kuwa hali hiyo inachangia visasi, chuki na kusababisha mauaji kwa wenye haki.

Mambo mengi yamesemwa na viongozi wa ngazi za juu kuhusu mwenendo mzima wa askari ndani ya jeshi la polisi hatua ambayo imesababisha jamii kwa ujumla kuwaona ni kama wanyang'anyi, wala rushwa na wauaji. Kwa ujumla, picha halisi ni kwamba wananchi wamekosa imani na jeshi la polisi hali ambayo si shwari kwa amani na utulivu ndani ya taifa.

Kama wahenga wasemavyo ukiona ngoma inavuma sana ujue iko karibu kupasuka. Maneno ya Rais pamoja na msisitizo wa IGP Sirro ni dhahiri kuwa taasisi hiyo ambayo inapaswa kuwa kioo katika utendaji kazi wake imepoteza dira na mvuto. Hakuna njia nyingine zaidi ya kujitathmini na kubadili mwenendo wake. Yaliyosemwa juu ya kubadilika yazingatiwe.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Shughuli za kiuchumi bila kuwa na hadhari ya corona ni hatari

Na Sabato Kasika

**TANGU** awali wakati ugonjwa wa corona unaingia nchini, serikali iliweka wazi msimamo wake wa kutowafungia ndani wananchi, badala yake ikaelekeza kuendelea na shughuli zao za kiuchumi, lakini wakiwa na tahadhari.

Kutokana na uamuzi huo, ikatoa mwongozo wa udhibiti wa ugonjwa huo, kwa lengo kwamba, wanapokuwa kwenye shughuli zao za kujitafutia riziki wawe wanauzingatia ili wasiambukizwe corona.

Mwongozo huo kupitia afua ya kuthibiti misongamano katika jamii bila kuathiri shughuli za kiuchumi toleo la kwanza, umeweka wazi jinsi ambavyo watu wanaweza kujikinga na ugonjwa huo.

Unawataka kuvaa barakoa katika vyombo vya usafiri na stendi za mabasi, daladala na bodaboda, huku vyombo vya ulinzi na usalama vikitakiwa kusimamia utekelezaji wa mwongozo huo.

Kwenye vituo vya mabasi, kunatakiwa kuwapo ndoo za maji tiririka ili abiria waweze kunawa kabla ya kupanda ndani ya vyombo hivyo vya usafiri, huku wakiwa wamevaa barakoa.

Aidha, mwongozo huo unahimiza wananchi kuepuka mikusanyiko isiyo ya lazima, lakini pia vyombo vya usafiri kama daladala na mabasi ya mikoani vinatakiwa kuzingatia idadi ya viti kwa kutojaza abiria kupita kiasi.

Hayo yote yanatakiwa kufanyika ikiwamo kuepuka mikusanyiko isiyo ya lazima, lengo likiwa ni kulinda afya za abiria na watu wengine kwa ujumla dhidi ya corona ambayo bado haijapatiwa tiba.

Pamoja na kuwapo kwa mwongozo huo, kwenye maeneo ambayo huwa ni lazima kuwapo kwa mikusanyiko ya watu kama sokoni, bado hakuna tahadhari inayochukuliwa ili kudhibiti kuenea kwa corona.

> **Pamoja na kuwapo kwa mwongozo huo, kwenye maeneo ambayo huwa ni lazima kuwapo kwa mikusanyiko ya watu kama sokoni, bado hakuna tahadhari inayochukuliwa ili kudhibiti kuenea kwa corona.**

Baadhi ya masoko kama ya Mbezi Mwisho, Dar es Salaam, hayana ndoo za maji tiririka, huku wateja na wafanyabiashara, wengi wao hawavai barakoa na pia hakuna ndoo za maji tiririka, ili kuwezesha watu kunawa.

Kwa mazingira kama hayo, ni wazi lengo la serikali la kutoa mwongozo wa kuwezesha Watanzania kuendelea na shughuli za kiuchumi huku wakiwa na tahadhari, linaweza lisifanikiwe kama watu wenyewe hawatajiongeza.

Ukigeukia upande wa usafirishaji wa abiria, huko nako ni vurugu tupu, kwani pamoja na kutakiwa kutojaza abiria kupita kiasi, daladala nyingi ni kama zimeuweka pembeni mwongozo huo.

Baadhi ya makondakta na madereva wameweka mbele utafutaji wa pesa kwa kujaza abiria kupita kiasi katika magari yao, badala ya kulinda afya zao na za abiria wao kama ambavyo mwongozo unaelekeza.

Abiria nao kwa upande wao hawaoni umuhimu wa kusubiri magari mengine wanapokuta yaliyopo yamejaa, wanapanda kwa madai kwamba, wanataka kuwahi katika shughuli zao, lakini pia hawavai barakoa

Ikumbukwe kuwa kufanya shughuli za kiuchumi bila tahadhari ya corona ni hatari, hivyo ingekuwa vyema kama kila mmoja kwa nafasi yake atafuata maelekezo kutoka katika mwongozo.

Kuzingatia mwongozo huku shughuli za kiuchumi zikiendelea, ni njia nzuri ambayo inaweza kusaidia Watanzania kuwa salama zaidi kuliko kujisahau na kujipa matumaini kuwa ugonjwa umeisha nchini.

# SAFU/MAKALA

## KWA MASLAHI YA TAIFA

# Krisimasi ni sikukuu ya kutoa na kuwakumbuka wenye uhitaji



Na Pascal Mayalla

LEO ni 'Boxing Day', ambayo huifuatia Sikukuu ya Krismasi. Bado tuko kwenye "festival mood" or "holiday mood" yaani hali ya sikukuu au ya kisherehe. Hii ni siku ya kufungua maboksi ya zawadi kutokana na utamaduni uliojengeka katika siku za nyuma.

Sijajua huku Afrika, na sisi Tanzania tukiwamo, ni wangapi wanafungua maboksi ya zawadi tulizopokea?! Kwa hali hii ya uchumi wetu, zaidi ya kula na kunywa na kujumuika pamoja, sijui kama 'Boxing Day' inasherehekewa kwa maana halisi ya kufungua zawadi. Hii ni kwa sababu wengi hatutoi zawadi na hatujitoi.

Kwa mwaka huu sikukuu hii imedondokea siku nzuri, wikiendi, Jumamosi na Jumapili. Tena nimekumbuka zile enzi za Mzee Rukhsa, Rais Ali Hasaan Mwinyi, sikukuu ikiangukia siku za mapunziko, yaani Jumamosi na Jumapili, mapumziko hayo yanafidiwa kwa mapumziko siku ya Jumatatu na Jumanne, kazini ingekuwa Jumatano!.

Sasa kutokana na hii mudi ya kisherehe sherehe na kusherehekea na kwa vile sikukuu yenyewe ya Krismasi ni sikukuu ya Kizungu, iliyoletwa Afrika na ujio wa Wamisionari wa Kizungu walioleta dini ya Kikiristo Afrika, kwenye kichwa cha habari cha makala hii kwa leo, nimeamua kuwatakia heri ya sikukuu ya Krismasi.

Japo Krismasi ni sikukuu ya kuadhimisha kuzaliwa kwa Masiha, Bwana Yesu Kristo, inaadhimishwa dunia nzima na watu wa dini zote na mataifa yote hata nchi za Kiislam, kwa kitu kinachoitwa 'Chirstmas Spirit is Giving', yaani dhima ya Krismasi ni kutoa, kujitoa, kukipelekea zawadi kichanga kilichozaliwa.

Hata hivyo, kwenye maisha yetu, si lazima kuwepo kichanga kilichozaliwa, hivyo huo moyo ni kutoa kwa waliotuzunguka ukianzia kwenye familia yako, majirani, ndipo twende kwa ndugu, jamaa na marafiki hadi kwa wazazi wetu vijijini. Ni sikukuu ya kutoa na si kupokea.

Tena ukitoa, toa kwa wote bila kujali ni wa dini gani maana Krismasi ni sikukuu ya wote. Hata simulizi za mwanzo wa ulimwengu kwa dini kuu mbili za Wakristo na Waislamu, sote tunakubaliana dunia iliumbwa na Mungu, mwanzo Mungu aliwaumba Adam na Eva (Kikristo) na Adam na Hawa (kiislamu), hivyo sisi binadamu wote ni watoto wa baba mmoja. Adam, hata neno mwanadamu au binadamu, maana yake ni Mwana wa Adamu au Bin Adam. Hata sisi nembo yetu ya Taifa yenye mwanamke na mwanamume, Bibi na Bwana, wale ni wazazi wetu, Adam na Hawa.

Kwa dini zote mbili kuu duniani, Wakristo na Waislamu, tunaamini kisa cha Nabii Abraham (Kikristo) Ibrahimu, (Kiislamu) na mkewe Sara (Kikristo), Sarai (Kiislamu), waliishi muda mrefu kwenye ndoa yao bila kubahatika kupata mtoto. Baada ya uzee kuwanyemelea na mkewe Sara siku zake kukoma, hivyo kutokuwa na uwezo tena wa kuzaa mtoto, ndipo akamtoa mjakazi wake wa Kimisri, Hagai (Kikiristu), Hagir (Kiislamu), kushiriki na mumewe Ibrahim, ili kuweza kupata mrithi.

Somo hapa ni familia ambazo hazikujaaliwa kupata watoto kutokana na tatizo la uzazi kwa mke, wanawake msiwe wachoyo kwa waume zenu, waruhusuni waume zenu kupata watoto kwa wanawake wengine. Hii ni endapo tatizo la uzazi ni kwa mwanamke, linapokuwa tatizo ni kwa mwanaume.

Baadaye kwa muujiza wa Mungu, mke wa Ibrahimu Sara, akiwa mzee wa umri wa miaka 80, alishika ujauzito, na kumzaa mtoto aliyeitwa Isaka (Kikristo), Isihaka (Kiislamu). Isumaili ndio Baba wa Waislamu wote, na Isaka ndio baba wa Wakisto wote. Ni katika ukoo huu ndio alikuja kuzaliwa Nabii Musa na aliyewakomboa Waisraeli kutoka utumwani Misri, na ndiye aliyepewa Amri Kuu za Mungu, ni zile zile amri alizopewa Musa, kupitia Torati na hata Yesu alipokuja, bado amri za Mungu ni zile zile. Yesu hakuja kuitengua Torati bali kuikamilisha, hivyo Wakristo na Waislamu ni watoto wa baba mmoja, tusherehekee Krismasi pamoja.

Kwa vile Krismasi ni sikukuu ya kizungu, wenzetu wazungu wanaisherehekea kwa kitu kinachoitwa "The Christmas Spirit" ambacho ni kusherehekea by "Giving" and not "Receiving", kumaanisha Krismasi ni sikukuu ya kutoa na si kupokea.

Kuna Watanzania wengi wanajiandaa kwa mwaka mzima, ikiwamo kuweka akiba ya fedha za kutumia kula Krismasi, wanajikuta wanaisherehekea kinyume cha malengo. Badala ya kutoa wao ndio kwanza wanatumia kwa kujipenda, kufanya matumizi makubwa na sherehe, kula, kunywa, kusafiri, kustarehe, kununua vitu na kujipa zawadi badala ya kuwapa zawadi wengine haswa wahitaji.

Mimi mwenyewe nimejikuta huwa ninatuma kadi tuu za Krismasi kwa watu na salamu za heri ya Krismasi kavu kavu bila kutoa zawadi yoyote kwa wahitaji. Hujiwekea akiba nzuri kwa ajili ya kusafiri na familia, kuinunulia familia nguo mpya za Krismasi, kula vizuri, kunywa kwa sana na kufurahi kwa kujifurahisha sisi na familia zetu, na ndugu zetu na jamaa zetu na marafiki zetu lakini je, tumewakumbuka wahitaji?.

Naomba japo sikukuu ilikuwa jana na kwa vile watu hatufanani uwezo, kipato na kuyawezea maisha, kwa vile sikukuu hii ni siku ya kutoa, hebu basi kwa wiki hii, waangazie majirani waliokuzunguka ni watu wenye hali gani. Wakumbuke wagonjwa hospitalini, wafungwa magezarani, yatima kwenye nyumba za yatima au watu wengine wenye uhitaji.

Hebu jitoe uwashike mkono kwa kidogo chochote kitu ili kudumisha "The Christmas Spirit, To give", kwa kujitoa kuwatolea chochote ili na wao pia washerekee sikukuu ya Krismasi ambayo ni sikukuu ya wote.

**Nawatakia Krismasi njema na Mwaka Mpya wenye mafanikio. Paskali.**

## MADONGO YA MGAGAGIGIKOKO

# Majina yetu haya yaendane na utamaduni wetu



Na Joseph Kulangwa

**Majina ya vitabu ndani ya Biblia ndiyo hayo tena ya Kizungu, kina Moses, kina Mathew, kina Jacob, kina Joseph na mengineyo mengine. Ulishasikia wapi katika Biblia kuna kitabu kinaitwa Masanja, Maregesi au Masatu?**

JAMANI poleni kwa uchovu wa jana. Bila shaka mnafungua zawadi mlizoletewa na ndugu, jamaa na marafiki, kama kweli zililetwa, kwa sababu Dunia ya leo kila mtu anajua nini kinaendelea kiuchumi.

Tunakaribia kumaliza mwaka na kuanza mwingine, ila tujiulize tulifanya nini na tunataka kufanya nini mwakani na Uviko yetu hii. Kama ni haya haya basi tujipange kwa haya haya, na kama ni mapya pia tujipange.

Zamani tilisimuliwa na wengine kushuhudia, jinsi watu walivyokuwa wanazaliwa na kupewa majina yao ya kienyeji. Mtoto alizaliwa akapewa jina la babu au bibi yake. Hiyo ilikuwa kurithishana.

Ili kurithisha na kufanya jina liwe endelevu, akizaliwa mtoto wa mtoto wake ataitwa kwa jina lake, ndiyo sababu haikuwa na si ajabu kumsikia mtu anaitwa Kulangwa Kulangwa au Majaliwa Majaliwa.

Walipokuja watu wakijifanya wajanja na wenye akili kuliko sisi, watu waliojigamba kuwa karibu na Mungu, wakijiita Wamisionari, walitulaghai kuwa wametumwa na Mungu kueneza Jina na Neno lake.

Nasi kwa akili tulizokuwa nazo tukawaamini, kwamba kweli kwa kuwa weupe kwa rangi lazima walikuwa wanaishi na Mungu huko walikotoka na kwa kweli walikuja kutwambia Mungu anatuonaje na anatutaka nini.

Waliposikia majina kama haya ya kienyeji, wakasema ni ya kishenzi, hayafai na kututafutia njia fulani hivi ya kuzika majina yetu, wakisema njia hiyo ni kubatiza. Yaani mtoto anazaliwa, anaitwa jina la babu au bibi, kisha anabatizwa na kuzika jina hilo na kupewa la kizungu.

Tukaanza kuwasikia akina John na Jane, kina William na Happy, tukawasikia kina Mama Happy, Mama John, Baba Willy na Baba Jane! Majina haya ya kwetu ikawa ndiyo baibai kabisa.

Walikuja kwa gia kubwa na vitabu vikubwa vikubwa vyenye rangi nyeusi wakiviita Biblia. Humo wakasema ndimo kwenye Neno la Bwana, humo kila kilichoandikwa ni cha kweli na ukikiuka ni dhambi na siku ya mwisho ni moto tu hakuna kingine.

Majina ya vitabu ndani ya Biblia ndiyo hayo tena ya Kizungu, kina Moses, kina Mathew, kina Jacob, kina Joseph na mengineyo mengine. Ulishasikia wapi katika Biblia kuna kitabu kinaitwa Masanja, Maregesi au Masatu?

Baba wa Taifa mwenyewe na ujanja wake wote akaitwa Julius, ili kuua Kambarage. Mpaka anakufa akafa na Julius lake hilo kutokana na kwamba alibatizwa akalipewa.

Mwenzake aliyekuwa anaitwa Joseph Desire pale Kongo Kinshasa, alipoona udwanzi akatangaza kubadili jina lake akajiita Mobutu Sese Seko Kuku Ngbendu wa Zabanga na nchi akaiita Zaire na pesa ikaitwa Zaire pia.

Watu wake walipoona uamuzi huo kuwa wa busara, nao wakabadili majina yao, kuna mwanamuziki aliyekuwa anaitwa Francis au Franco, akajiita Luambo Luanzo Makiadi Lokanga Lwadjo Pene.

Wenzake walipoona hivyo, nao wakabadili majina huku wakitupilia mbali ya Kizungu, wakabaki wana wa Zaire na majina ya Kizaire, ingawa baadaye tena wakakengeuka wakaja viongozi wengine na kutupilia mbali mabadiliko hayo ya kijana dume.

Nchini kwetu pia zamani tulikuwa na wanamuziki wenye majina yao tu kama vile Mbaraka Mwinshehe, kina Juma Kilaza, kina Wema Abdallah, Patrick Balisidya, na wengineo wengi.

Ingawa majina yao yalifanana fanana ya Kiarabu hivi, lakini yaliendana na Kiswahili ambayo ni lugha yetu adhimu, na yalitamkika kwa wazee,vijana na watoto bila matatizo na ni majina waliyopewa na wazazi wao.

Leo kumezuka wimbi la majina kupewa watoto, majina magumu magumu na si magumu tu bali ya kigeni. Unasikia kazaliwa mtoto anaitwa Skylar, Brian, na kadhalika. Yote hiyo ni kuabudu uzungu na kutweza uafrika na hasa utanzania wetu.

Ona wasanii na wanamuziki wa leo wa kizazi hiki tunakiita kipya. Hivi kweli mtu una badili jina lako unajiita eti Diamond Platnumz, Mtanzania wewe, eti Harmonize, Harmorapa, Cindy, Nandy! Kisa nini? Uwe mzungu au? Muziki wenyewe sasa utuimbie wa Nigeria, Afrika Kusini!!

Kwani ukiendelea kuitwa Ali Kiba, Abdul Kiba, Shilole, Khadija Kopa. Utapungukiwa nini katika maisha yako? Muziki wako utapotea au? Hebu jamani mwaka mpya tubadilike turudi kwenye jadi yetu, tuachane na ulimbukeni. Hamkuchoka mlivyofanywa na Wamisionari? Siku kuu njema ya makasha!

**Alamsiki!**

## KONA YA UKWELI

# Viongozi maagizo yenu yanachanganya watumishi



Na Thobias Mwanakatwe

UTUMISHI wa umma ni mfumo wa kiutawala na kimenejimenti uliokabidhiwa jukumu la kuhakikisha jamii inapata huduma inayokusudiwa kutoka kwa serikali au taasisi yoyote kwa niaba ya serikali kwa kuzingatia sera, sheria, kanuni, taratibu na miongozo mbalimbali.

Pamoja na kuwapo kwa sera, kanuni na sheria zinazosimamia watumishi wa umma katika siku za hivi karibuni, kumeibuka baadhi ya viongozi kwa makusudi kukiuka sheria kuwakandamiza watumishi.

Miongoni mwa haki ambazo zipo kisheria zilizoanza kukiukwa na baadhi ya viongozi ni kupiga marufuku likizo za watumishi wakati inafahamika kuwa suala la likizo ni jambo la kisheria ambalo kila mtumishi anapaswa kupewa.

Nimeanza kwa kuyasema hayo kwa sababu Desemba 7, mwaka huu, Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, alinukuliwa na vyombo vya habari akitangaza kufuta likizo kwa watumishi wote wa serikali mkoa huo ambao idara zao zinahusika na ujenzi wa vyumba vya madarasa.

Katika kusisitiza hilo, alisema hatapokea barua za likizo pasipo kupata taarifa za kukamilika kwa ujenzi wa miradi ya madarasa, madawati na maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya wafanyabishara wadogo maarufu kama machinga.

Lakini katika hali ambayo naiona ni ya kujichanganya na kuwachanganya watumishi baada ya tamko hilo la RC Mbeya, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mohamed Mchengerwa, naye akatoa tamko kuhusu likizo za watumishi.

Akasema likizo ni haki ya mtumishi kisheria, hivyo hakuna haja ya Kiongozi kuzuia haki hiyo isipokuwa kwa sababu maalumu ambayo mtumishi husika atashirikishwa.

Mchengerwa alisisitiza kuwa kiongozi anapotaka kuzuia likizo ya mtumishi, afuate taratibu ambazo ni pamoja na kuzungumza na mtumishi husika anayetaka kuchukua likizo, ama kwa kumlipa gharama za kuzuia likizo hiyo au kumsogezea muda wa kuchukua likizo hiyo.

Mchengerwa alifafanua kuwa ni vizuri kuzungumza na mtumishi kwa kutumia lugha nzuri na akakuelewa kuliko kutumia cheo ulichonacho au lugha kali kwani unaweza ukazuia likizo yake na asifanye kazi inavyotakiwa.

Tamko hilo la Waziri wa Utumishi liwe somo kwa viongozi wengine wasifikiri kuwa likizo za watumishi ni ombi bali watambue kuwa ni suala ambalo lipo kisheria.

Viongozi lazima wafahamu kuwa kila mtumishi wa umma anastahili au anatakiwa kupewa likizo ya siku 28 kwa kuzingatia mzunguko wake wa likizo (leave cycle) na anastahili kulipwa nauli mara moja ndani ya mzunguko wa likizo wa miaka miwili. Katika hali ya kawaida hakuna mtumishi anayestahili likizo ya mwaka kabla ya kutimiza miezi minane tangu kuajirwa kwake.

Mzunguko wa likizo unaanzia tarehe ambayo mtumishi aliajiriwa kwa mara ya kwanza isipokuwa kwa watumishi walio katika masharti ya mkataba.

Wakuu wa mikoa lazima watambue kuwa moja ya majukumu yao ni kuhakikisha uwepo wa Haki na Sheria katika mikoa yao, kuongoza na kusimamia operesheni za maafa na kufariji.

Pia RC kama Mwenyekiti wa Kamati ya Ushauri ya Mkoa (RCC), atawajibika kufanya jitihada za kuhakikisha kutimizwa kwa sera za serikali juu ya mkoa husika na kufanya yale yote yatakayosaidia kuimarisha ulinzi na usalama wa mkoa kwa ushirikiano na serikali za mitaa.

Viongozi watambue kuwa haki za watumishi wa umma ni jambo au kitu ambacho mtu anapaswa apate kutoka kwa mtu mwingine au kutoka kwenye mamlaka fulani, inaweza kuwa miongoni mwa yale yaliyotajwa kwenye Katiba, sheria, kanuni, maagizo au maelekezo mbalimbali, haki ni lazima kutimizwa au kutolewa na isipotolewa au ikikiukwa hudaiwa.

Wakati mwingine kutotimizwa haki kunaweza kusababisha mgogoro na mgongano kati ya mwenye haki na anayepaswa kuitoa au kuitimiza na kwa watumishi wa umma haki zao ni kama vile maslahi mbalimbali, mafunzo, kupandishwa cheo, kuheshimiwa, kuthaminiwa, kusikilizwa, kushirikishwa, kurekebishwa na kuadhibiwa.

**MUNGU IBARIKI TANZANIA, MUNGU WABARIKI WATUMISHI WA UMMA**

**Kwa maoni na ushauri tumia barua pepe mwanakatwe2005@yahoo.com**

## DARASA LA NDOA

# ATHARI ZA MIGOGORO YA NDOA KWA WATOTO KABLA NA BAADA YA KUZALIWA -1



Na Mch.Dk. Enock Mlyuka

TUNAPOZUNGUMZIA suala la watoto ni muhimu kufahamu kuwa mtoto ni nani. Kwa mujibu wa Sheria ya Tanzania, mtoto ni mtu yeyote aliye na umri chini ya miaka 18. Ifahamike kuwa, watoto ni zawadi ya thamani kutoka kwa Mungu.Zawadi hii inahitaji kutunzwa, kulelewa na kulindwa.

Wazazi wengi leo hawana muda na watoto wao. Watoto wengi wanajilea wenyewe na wengine kulelewa na watu wengine kwa sababu ya wazazi wao kutowajibika ipasavyo. Baadhi ya wazazi wamefanyika viwanda vya kuzalisha watoto pasipo kuwajibika katika malezi na matunzo. Hali hii inaathiri sana makuzi na maendeleo ya mtoto au watoto.

Watoto ni binadamu wenye hisia. Hisia zao hutegemea na kile kilichowekezwa katika ubongo wao. Fikra za mtoto huishia kwa kile anachokiona na kusikia. Kwa hiyo, watoto hujifunza haraka zaidi kwa kuona na kusikia. Ndoa na familia ni kitalu na shule ya kwanza ya malezi na makuzi ya mtoto.

Tabia na mienendo inajengwa katika familia. Wanasaikolojia wanasema, zaidi ya asilimia 60 ya mtu alivyo leo ni matokeo ya makuzi wakati wa utoto. Kwa maneno mengine, wewe na mimi tulivyo leo ni zao la utoto wetu. Mtoto mwenye malezi mabaya ni mzigo wa baba na mama yake sasa na baadaye.

### Hali ya migogoro

Ndoa ni zawadi ya Mungu kwa mwanadamu na kitovu cha familia, jamii, taifa na malezi. Mungu alianzisha taasisi ya ndoa ili watu waingie, waipende na kuifurahia. Hata hivyo, mambo yamekuwa kinyume kwa baadhi ya wanandoa. Siku hizi tunashuhudia migogoro mingi ya ndoa na kuvunjika kwa ndoa nyingi. Kwa baadhi ya familia, ndoa imegeuka kuwa jela ya nyumbani na kusababisha upotoshwaji mkubwa juu ya kusudi na maana halisi ya ndoa na familia.

Migogoro ya ndoa huondoa hisia za mapenzi na mvuto, hali hii huchangia uwapo wa vitendo vya ukatili ndani ya ndoa na vifo. Vyombo vya habari vimekuwa vikisikika kutoa habari za vitendo vya mauaji ndani ya ndoa katika baadhi ya maeneo hapa nchini.

Pia migogoro ya ndoa huathiri afya na ustawi wa familia. Athari hizi haziwahusu wanandoa tu, bali wazazi ambako wanandoa hao wanatoka pia. Athari za migogoro ya ndoa ni kubwa zaidi kwa watoto waliozaliwa katika ndoa hizo kwani huathiri sana makuzi na kusababisha msongo wa mawazo wenye athari mbaya (stress-leading to negative effects) kama inavyoelezwa katika sehemu zinazofuata.

### Athari kwa watoto

Migogoro ya ndoa na kuvunjika ni mbegu ya uharibifu kwa watoto kwani inawabomoa badala ya kuwajenga. Migogoro ya ndoa huleta athari zifuatazo;-

### Kisaikolojia

Huleta msongo wa mawazo kwa mtoto au watoto. Mfumo wa maisha ya mtoto unavurugwa. Mtoto au watoto wanapoteza mwelekeo wa maisha yao. Hujifunza kuwa maisha ya ndoa ni shida, hivyo wakiwa watu wazima wanakuwa hawapendi kuoa au kuolewa kwa sababu ya maisha waliyoyaona ya baba na mama yao.

Hali hii inatokana na hofu iliyotengenezwa ambayo husababisha kutafsiri ndoa kuwa ni utumwa na mateso. Watu wenye uzoefu huu wa maisha pale wanapoamua kuoa au kuolewa hutamani kuishi na watu wenye upendo sana, huruma, kujali na kuthamini kwa kiwango kikubwa ili kufidia pengo hilo la malezi ya huko nyuma. Bahati mbaya wakipata mtu au watu wasio na sifa hizo kinyume na matarajio yao, inakuwa ni vigumu sana kuvumilia changamoto za uhusiano pale zinapojitokeza.

Kadhalika, migogoro ya ndoa husababisha hali ya kutojiamini kwa watoto (inferiority complex). Watoto wanajiona ni watu wenye mkosi kuwa na wazazi wa aina hiyo katika jamii na kuona watoto wa wengine wako vizuri na wenye bahati. Mtoto anaanza kukata tamaa ya maisha na kujiona hana thamani katika jamii, hali inayopelekea baadhi ya watoto kuchukua maamuzi magumu ya kujiondoa uhai (commit suicide).

Kama migogoro ilikuwapo tangu mimba ilipotungwa, migogoro huweza kusababisha mimba kutoka na mtoto kufa hivyo kukatisha haki ya mtoto ya kuishi. Kama amezaliwa, anazaliwa mtoto mwenye maumivu na machungu katika nafsi (trauma) ambayo ameyapata wakati akiwa tumboni mwa mama yake.

Mtoto aliyezaliwa anahisi kukataliwa na kutokupendwa. Wapo watoto ambao wamejeruhiwa na kuumizwa wakiwa katika matumbo ya mama zao (prenatal development). Hali hii huathiri afya ya akili na maendeleo yao (mental and intellectual development).

Udumavu wa akili na upeo mdogo wa kufikiri na kuchakata mambo hujitokeza. Kama mtoto anasoma shule, ufaulu wake unashuka na wengine kufikia hatua ya kutokupenda shule na kisha kuacha masomo. Wako watu wenye matatizo ya afya ya akili tangu utoto wao bila wenyewe au wazazi wao kujua.

### Kibailojia

Watu wengine walimeharibika kutokanana na uzoefu mbaya waliopata kutoka kwa wazazi wao wakati wa utoto (negative parenthood experience). Watu wengine wamerithi roho za visasi,ugomvi, kuucha na kuachika, chuki, fitina, hasira kali (very emotional), kukosa staha na utaratibu na kusababisha kuwa na kizazi cha watu wakatili katika jamii. Wazazi wanakuwa wamezaa watoto wa aina yao.

Hali hii hujitokeza kwa sababu katika makuzi yao, watoto hawajawahi kuona matendo mema ya baba na mama yao. Matokeo yake watoto hawa wakiwa watu wazima na wao wanafanya vivyo hivyo, kwani ndicho walichokiona na kujifunza kutoka kwa baba na mama yao. Wanakuwa watu waliotengenezwa kuwa hivyo walivyo. Watu wa aina hii wanapopata nafasi za uongozi au wakioa na kuolewa huwatendea binadamu wenzao mambo magumu sana ya kuumiza mara nyingi.

**Itaendelea Jumapili ijayo**

**Dk. Mlyuka ni Mkurugenzi Mtendaji wa Tanzania Marriage and Child Care Foundation (TaMCare), asasi inayojishuhulisha na masuala ya ndoa, familia na malezi. Kwa maelezo zaidi, tembelea www.tamcare.or.tz. Fuatilia mafunzo zaidi katika tamcaretv online. Kwa maoni na ushauri wasiliana naye kwa: info@tamcare.or.tz au +255744000066.**

# MAISHA

DESEMBA 26, 2021

Nipashe

Baba, Mama na Mwana

Jumapili




Ukurasa 13


**2021 vifua vilitosha**



Ukurasa 15

## MAISHA NI NYUMBA

Ifanye nyumba pawe nyumbani



## HARUSI

Ukurasa 12




# Pambo la hereni zaidi ya hereni

Ukurasa 14


## MAJIBU YA WIKI ILIYOPITA






| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| ■ | D | U | N | D | A |
| ■ | U | ■ | ■ | E | ■ |
| U | M | A | ■ | R | ■ |
| ■ | A | ■ | B | E | I |
| ■ | Z | ■ | ■ | V | ■ |
| W | A | N | G | A | ■ |

## AMSHA AKILI





## FUMBO TOTO



Jaza maneno yafuatayo katika vyumba vilivyopo wazi:
IPO, IMO, JENGA, PWANI, NYUMBA, POPOTE


## TOA TOFAUTI 5



## WATOTO

# PAKA RANGI




Alichokifanya daktari

MTOTO Juma alirudi shuleni mapema kwa ajili ya kujiandaa na masomo ya kesho yake. Alikuwa na sura yenye mashaka kiasi ambacho mama yake alimgundua kuwa hayupo sawa.

Mama yake alimfuata hadi pale alipo na kuanza kumuuliza maswali.

**Mama:** Juma mbona nakuona haupo sawa mwanangu?

**Juma:** Kuna kazi katupa mwalimu tueleze maana yake, lakini pale naona kuna tezi na ile sabuni ya unga tu.

**Mama:** kazi gani na inasemaje?

**Juma:** Katuambia kuwa 'Mwenda tezi za omo, marejeo ngamani' si unaona hapo ndo najifikiria.

**Mama:** Huo msemo ni wa kale na una maana kwamba kila unapokwenda kutafuta kitu, lazima utarudi pale ulipo ukiwa unacho au huna.

**SWALI**

Taja wadudu watatu wanaosababishia magonjwa binadamu

## MAISHA NDIVYO YALIVYO

Na Flora Wingia



# Yajue mambo makuu mawili yaliyo mbele yako

***KARIBU** tena msomaji wangu tujumuike pamoja katika safu yetu hii tunapokaribia ukingoni kabisa kumalizia mwaka huu 2012. Wakati pia tunausubiria kwa hamu mwaka mpya 2022, nikupe siri mambo makuu mawili yaliyo mbele yetu.*

Siku zote uifahamu siri hii, kwamba katika maisha yako huko mbele kuna vitu viwili. Kwanza, mbele yako kuna 'Baraka kubwa'. Haijalishi leo unapitia hali gani ngumu kimaisha, iwe ni kupitia umasikini, au magonjwa. Mtu mwenye imani huona mafanikio yaliyo mbele yake.

Mungu mwenyewe aliweka siri hiyo kwenye neno lake pale aliposema, "kwa maana nayahesabu mateso ya wakati huu wa sasa kuwa si kitu kama utukufu ule utakaofunuliwa kwetu". Baraka zetu zipo, lakini hatumuulizi Mungu atufunulie tuzione. Muulize nifanye nini nizione Baraka zangu?

Kitu cha pili ambacho kipo mbele yako ni, 'Hatari kubwa'. Huu ndio ukweli kabisa kwamba ipo hatari kubwa mbele yako. Kusema hivi haina lengo la kukutisha msomaji wangu, la hasha! Ni ili uchukue tahadhari mapema.

> **"Unaweza ukawa na watoto wenye tabia njema lakini baadaye wakabadilika na ukaanza kuhuzunika. Kumbe ungechukua tahadhari mapema hayo yasingetokea.**

Ni ukweli kwamba ukiifahamu siri hii utajiweka sawa na kujipanga jinsi ya kukabiliana na lolote. Maadui zetu siku zote huwa wanajipanga ili kutuharibia mafanikio yetu siku za mbele. Kama wewe ni tajiri, ni muhimu uwe makini na siku zinazokuja.

Siyo hiyo tu, pia kama wewe una afua nzuri ujipange kwa siku za baadaye. Kama bado una ndoa nzuri jipange kwa baadaye kwani wengi walianza vizuri lakini mwisho ukawa mchungu.

Kama wewe ni mtumishi wa Mungu na una huduma nzuri, jipange kwa ajili ya siku za usoni kwani wengi walianza vizuri kwenye utumishi wao mwisho ukawa wa aibu. Unaweza ukawa na watoto wenye tabia njema lakini baadaye wakabadilika na ukaanza kuhuzunika. Kumbe ungechukua tahadhari mapema hayo yasingetokea.

Msomaji wangu, kama wewe ni tajiri, chukua tahadhari mbeleni kwani wengi walilala matajiri wakaamka masikini. Mungu mwenyewe alishaweka tahadhari pale aliposema, siku zinakuja, laiti ungalijua, hata wewe katika siku hii yapasayo amani.

"Lakini sasa yamefichwa machoni pako. Kwa kuwa siku zinakuja, adui zako watakapokujengea boma likuzunguke, watakuzingira pande zote, watakuangusha chini wewe na watoto wako, wasikuachie jiwe juu ya jiwe, kwa sababu hukutambua majira ya kujiliwa kwako"!

Hiyo ni tahadhari aliyoiweka Mungu mbele yetu tunayopaswa kuijua. Ni mambo yaliyofichwa lakini yapo mbele ya macho yetu ila hatuyaoni. Historia inaonyesha kwenye mwaka 70 AD mfalme Tito alishambulia Yerusalemu akaangamiza watu wengi, na wanawake waliokuwa na mimba walichanwa matumbo na kutolewa watoto.

Yalitokea mambo mabaya sana. Huzuni ni kwamba wale wenyeji wa Yerusalemu macho yao yalikuwa yamefichwa, hawakuweza kuona hatari itakayokuja mbele yao. Kama Mungu angekuonyesha ajali iliyoko mbele yako usingekubali kusafiri. Pia watu wengi wanajiingiza kwenye biashara ambazo zinakuja kuwaletea matatizo makubwa. Lakini kama wangeona mbele wasingeingia kwenye biashara hizo. Jifunze kumuomba Mungu akuonyeshe hatari iliyopo mbele yako!

Hebu sikia ushuhuda huu. Kaka mmoja alitaka kuoa lakini kabla ya kufunga ndoa walikwenda kwa muombaji mmoja mwanamke. Lengo ni kutaka kufahamu mapenzi ya Mungu kuhusu hatma ya uchumba wao. Baada ya maombi ya siku nyingi, yule muombaji aliota ndoto akaona ua zuri lipo kwenye maji machafu.

Alipotoa tafsiri kwa wale vijana hawakuamini. Kumbe tafsiri yake ilikuwa, ua ndiye yule dada lakini maji machafu ni yule kaka damu yake ilikuwa na virusi vya ukimwi. Yule mwombaji alipowaeleza walikataa kabisa tafsiri ya ndoto. Baada ya kulazimisha kufunga ndoa, siku za mbele wote wawili waliugua na kufa. Laiti kama wangetii ushauri ule.

Kumbuka ni sheria kwamba usipomuuliza Mungu hawezi kukuonyesha na hili wengi hawataki kulifahamu, wanaishia kusema Mungu unajua litakalotokea. Ni kweli anajua jambo lolote mbele yako, lakini ni mpaka unyenyekee kwake kwa maombi na kutii ndipo atakapokuonyesha.

***Bila shaka msomaji wangu umejifunza jambo hapo. Tukutane tena wiki ijayo. Kwa maoni, Ushauri tuma ujumbe mfupi kupitia 0715268581.***

## NAWAZA KWA SAUTI

Na Salome Kitomari



# Tusherehekee Krismasi, Mwaka Mpya tukiweka akiba ya 2022

JANA Watanzania hasa Wakristo waliungana na wenzao duniani kusherehekea kumbukumbu ya kuzaliwa kwa Yesu Kristo, ambayo inaambatana na kuuaga mwaka 2021 na kuukaribisha 2022.

Kipindi hiki, walio likizo hupenda kujumuika na familia zao kwenda vijijini au kwenye miji au vivutio mbalimbali ndani na nje ya nchi kupumzika au kusalimia ikiwa ni namna ya kukaa na kufurahi pamoja.

Wakati huu usafiri wa kwenda mikoani huwa ni tatizo kubwa kama ilivyoonekana wiki iliyopita, mamia ya abiria walijikuta kwenye wakati mgumu kutokana na ulanguzi wa nauli pamoja na kukosa magari kiasi cha kutumia usafiri binafsi au mbasi yaliyopewa vibali maalumu kwenda mikoa hiyo.

Mikoa yenye changamoto kubwa ni Kanda ya Kaskazini kutokana na idadi kubwa ya wasafiri na hali huwa mbaya tena mwanzoni mwa Januari wakati wengi wanarudi kwenye mikoa yao hasa Dar es Salaam.

Kipindi hiki ni lazima kusherehekea kwa kuwa na akiba ya ada za watoto ambao wanatakiwa kurudi shule Januari, kodi za nyumba na mahitaji mengine muhimu ya familia.

Kubwa zaidi ni kuhakikisha familia inabaki salama hasa kwa watakaotumia usafiri binafsi kwenda likizo kuhakikisha wamekagua magari yao, kuwa na madereva sahihi wenye kuzimudu na kuheshimu sheria za usalama barabarani.

Kwa wale wanaopenda kupeleka au kuwaacha watoto kwenda kutembea sehemu mbalimbali hasa kwenye fukwe wanaambatana na watu wazima ili kuhakikisha usalama wao.

Kwenye maeneo hayo watoto hufanyiwa matukio mabaya na wengine ni rahisi kuzama baharini, ni lazima kila mzazi awajibike kuhakikisha usalama wa watoto wao wakati wote.

Kila mwisho wa mwaka, Jeshi la Polisi linapotoa takwimu huonyesha kuongezeka kwa ajali au uhalifu mwingine, huku vituo vya TV vikiwa na idadi kubwa ya watu waliopotea wanatafutwa na ndugu zao.

Hii iwe fundisho na tuone mabadiliko kwenye sikukuu hizi kwa kila mmoja kutimiza wajibu wake, kwa kuwa usalama wa watoto ni wajibu wa mzazi vinginevyo ni kuwaumiza pasipo sababu.

Ni muhimu sana wakati huu kufuatilia kwa karibu disco toto zinazoandaliwa kwenye mitaa mbalimbali, lazima kuwe na usalama wa kutosha ili kuepusha majanga na kuharibika kwa watoto.

Pia Jeshi la Polisi liendelee kutimiza wajibu wake wa kuwalinda watu na mali zao, kwa kuwa wapo ambao hutumia mwanya wa mapumziko ya sikukuu kufanya uhalifu kwa kuamini hawatakamatwa.

> **"Mwaka 2022 uwe wa mabadiliko makubwa hasa kwa kuangalia wapi tulijikwaa, sababu za kujikwaa na wapi tulikoangukia na namna ya kusimama na kusonga mbele.**

Kufanikisha sherehe hizo kunahitaji ushiriki wa kila mmoja kuanza na usalama wake, familia yake na watu wa karibu, mtaani kwake, kata, wilaya, mkoa na taifa ili kuhakikisha wote tunavuka salama.

Kipindi hiki kiwe cha kuendelea kuimarisha umoja wa familia hadi taifa ili kuwa na amani ambayo ndiyo kitu kikubwa na cha msingi kwa kila mtu huku tukimtanguliza Mungu muweza wa yote.

Mwaka 2022 uwe wa mabadiliko makubwa hasa kwa kuangalia wapi tulijikwaa, sababu za kujikwaa na wapi tulikoangukia na namna ya kusimama na kusonga mbele kutoka hapo.

NI muhimu kuanza na mipango maalumu kwa mwaka mpya na namna ya kuifikia ili kuwa na maisha mazuri kwa kuwa jambo lolote linafanikiwa kwa kuwa na mipango thabiti.

# HARUSI



ILIKUWA harusi ya kipekee kati ya bwana Amani Magelanga na Anna Siwonike, iliyofungwa Desemba 4, mwaka huu katika ofisi ya Mkuu wa wilaya ya Iringa na kufuatiwa na sherehe ya aina ake iliyohudhuriwa na watu mashuhuri na viongozi mbalimbali wa serikali.











MITINDO

# 2021 vifua vilitosha

MWAKA 2021 umetumika vyema na baadhi ya wanaume kujenga miili yao kiafya na kuweka mvuto wa kipekee.

Lakini jambo la kipekee kujenga mili katika hali ya mazoezi ni njia nzuri ya kufanya kila nguo wanazovaa ziwakae vyema.

Ndani ya mwaka huu, katika majengo ya mazoezi maarufu kama Gym au maeneo ya wazi ya mitaa, watu wamekuwa wakijitokeza kwa wingi kuweka miili yao sawa.

Ukweli ni kwamba ukiwa na mwili wenye misuli na uliokaa vizuri, kila unapovaa nguo iwe suruali, shati au fulana kila mtu anapenda kukuangalia.

Kizuri zaidi hata katika suala la mahusiano, wanaume wenye miili ya kukata kiasi anakuwa na mvuto zaidi kwa wanawake na hilo pekee linawafanya vijana wengi kukimbilia kufanya mazoezi.

Vijana wengi wamejikuta wakiingia katika mtindo huo na kuvaa nguo ambazo ziliwaonyesha mikato ya vifua vyao, mikono na wakati mwingine ile ya tumboni maarufu kama Sixpack.











UREMBO



# Pambo la hereni zaidi ya hereni



HERENI ni pambo linalovaliwa masikioni na kwa kiasi kikubwa linachangia kuongeza mvuto na muonekano wa mwanamke.

Kuna aina nyingi za hereni katika tamaduni mbalimbali. Zipo ambazo hutengenezwa kwa kutumia vito vya thamani kama vile Dhahabu, Almasi, Shaba au Kopa.

Vilevile zipo ambazo hutengenezwa kwa kutumia malighafi za asili kama vile ubao, vifuu vya nazi, mfupa, kioo na shanga ambazo zimekuwa zikivaliwa sana na wanawake wa kimasai. Hereni zilizotengenezwa kwa shanga zimekuwa zikiwavutia watu wengi kuvaa kutokana na nakshi zake za asili.

Mara nyingi uvaaji wa hereni unatakiwa kuzingatia aina ya nguo uliyovaa, hapo unatakiwa kucheza na rangi.

Mpangilio wako wa nguo na hereni hata na viatu utakufanya uonekane maridadi muda wote.

Unapotoka kwenda katika shughuli zako, au uwapo nyumbani basi zingatia uvaaji wa hereni na nguo. Uvaaji usiozingatia mpangilio wa rangi na hereni zako huondoa ladha ya urembo na si rahisi kwa mtu mwingine kugundua umependeza.

Licha ya kuwa hapo awali hereni zilikuwa zikivaliwa na wanawake pekee, lakini miaka ya hivi karibuni tunaona urembo huu unaanza kuwavutia baadhi ya wanaume hususan vijana wa mjini.

Kutokana na hilo kuna hereni ambazo zimetengenezwa maalumu kwa kuvaliwa na wanaume, hizi huwa za kubana na huwa na umbo dogo ukilinganisha na zile zinazopendwa kuvaliwa na wanawake.

Epuka kuvaa hereni zaidi ya moja katika tundu la sikio kwani kufanya hivyo kunaweza kupelekea ukubwa wa tundu kuongezeka na hatimaye nyama ya sikio kuchanika.

Hereni nzito sana nazo huchangia kutokea kwa tatizo.

MAPISHI

Na Mary Geofrey

# Furahia X-Mass na saladi ya soseji

WAKATI tukiendelea kusherehekea Sikukuu za Krismasi na Mwaka mpya, ni wazi watu wamekuwa wakila vyakula vingi ambavyo kimsingi vinashibisha tumbo.

Ili kupunguza tatizo la kuongeza mwili wakati wa sikukuu ni muhimu kutumia vyakula vyenye faida kiafya kama saladi ambayo itakusaidia kufanya ule chakula kidogo.

Salad ni chakula chepesi, kinakupa nguvu za kutosha na kuzuia adha zinazotokana na kushiba kupita kiasi.

Salad hii ina nyama kiasi ambayo inaweza kukupa nguvu zaidi, hasa kwa wale wanaopenda kula nyama katika kila mlo.

**MAHITAJI**

Kabichi, nyanya, vitunguu,spinach, pilipili hoho, mafuta ya Oliva, limao au vinegar au ndimu, chumvi kiasi na sausages



**NAMNA YA KUANDAA**

Anza kuandaa soseji kwa kuzichemsha na maji, weka chumvi kiasi na acha ziive. Kata mboga za majani kwenye vipande vidogo na weka kwenye sahani.

Kata nyanya, pilipili hoho, karoti kwenye vipande vidogo, kisha changanya na salad yako.

Kata soseji kwenye vipande vidogo na changanya kwenye saladi

Changanya vinegar, limao au ndimu na mafuta ya mzaituni pembeni kwenye bakuli. Unakoroga vizuri hadi ziwe sawia.

Nyunyizia mchanganyiko wa limao au ndimu au vinegar na mafuta juu ya salad. Nyunyizia kuzunguka saladi, isijirundike sehemu moja.

Weka chumvi kiasi kisha anza kuchanganya changanya

Kumbuka, saladi inaliwa ikiwa ya baridi, hivyo huna haja ya kupasha moto.

Endelea kusherehekea sikukuu kwa kula chakula bora.

MAISHA NI NYUMBA

Na Elizabeth Zaya



# Ifanye nyumba pawe nyumbani

## Namna ya kupanda miti ya mapambo katika eneo dogo



BAADHI ya watu nyumba zao zina maeneo madogo, wanashindwa kuweka mandhari ya kupendeza kwa kuhofia kutokuwa na sehemu ya kupumzika.

Hata hivyo, suluhu ya tatizo hilo ipo kwani unaweza kutumia eneo dogo kwa kupanda miti na kisha kupata eneo la mapumziko na ukafurahia maisha.

Zifuatazo ni dondoo za namna ya kupanda miti ya mapambo katika eneo dogo.

**1:** Plum yenye majani mekundu (Prunus cerasifera var. pissardii), ni aina ya mti ni mti wenye majani ya zambarau unafaa kupandwa katika eneo dogo. Mti huu unafikia hadi mita 15, lakini kwa kawaida unakuwa na mita sita.

Wakati wa baridi hutoa maua meupe na unapendeza unapokuwa nje.

**2:** Pitosporo (Pittosporum tobira) ni mwingine ambao unaweza kutumika kama pambo nje ya nyumba na kuleta taswira nzuri. Urefu wake unafikia mita saba na majani yake ya kijani kibichi na wakati wa mvua hutoa maua meupe na yenye kunukia.

**3:** Mti wa Lilo (Syringa vulgaris), una majani ya kijani na unafikia urefu wa mita saba. Una matawi kuanzia katika shina lakini inavumilia kiangazi na katika kipindi cha mvua hutoa maua meupe au mekundu.

MIONGONI mwa maeneo ambayo huwa ni faraja na ya kupumzisha akili baada ya shughuli nyingi ni nyumbani.

Nyumbani ndipo palipo na mkusanyiko wa maisha, kumbukumbu na upendo kwa asilimia kubwa ya watu.

Binadamu kila mmoja hujishughulisha na mambo mbalimbali lengo likiwa ni kujitafutia ridhiki na kuhakikisha mkono unakwenda kinywani na mambo mengine ya kifamilia yanakwenda sawa.

Pamoja na kujishughulisha huko, mwisho wa siku lazima arejee nyumbani kujipumzisha bila kujali umbali wake.

Hivyo basi, kwa vyovyote vile lazima uhakikishe nyumbani panakuwa mahali sahihi, panapokupa furaha na panafanyika kuwa nyumbani kweliikweli.

Katika kipindi kama hiki cha mwisho wa mwaka, wengi hupenda kuchukua mapumuziko ya kikazi, kwa hiyo ili kutengeneza mwanzo mzuri wa shughuli zake kwa mwaka unaofuata ni muhimu kuhakikisha nyumbani panafanyika pa faraja, amani na furaha.

Si tu kwa utulivu, lakini panawekwa vizuri kimazingira na kuwapo na madhari ya kuvutia mtu kupumzika. Zipo njia mbalimbali za kufanya ambazo hazihitaji gharama kubwa ya kifedha ambazo ni rahisi na ni vitu vidogo vidogo.

Mojawapo ni mapambo. Ndani ya nyumba yako unaweza kutafuta baadhi ya picha za mapambo ambayo unayapenda na ukapamba.

Tumia pia picha nzuri ziwe za kuchora au zinazoonyesha alama ya upendo au yoyote inayokukumbusha enzi zile ukiwa nyumbani kwenu ulikozaliwa.

Ipe nyumba yako mwonekano na hisia inayotambulisha familia au aina ya watu wanaoishi katika nyumba husika au familia uliyowahi kuwa nayo awali.





Hakikisha mwonekano wa nyumba haufanani siku zote hususani ndani kuanzia sebuleni, vyumba vya kulala na hata nje kwenye mpangilio wa maua kwa wale wenye nafasi kubwa.

Kila nyumba ina upekee wake na mahitaji tofauti kuendana na wakaaji wake.


Pia usafi ni jambo jingine la kuzingatia ambalo linapaswa kuzingatiwa katika kuweka mazingira yake kuwa ya kuvutia kukaa wakati wote.

Bila kusahau suala la mapishi, ili nyumbani au mtu ajisikie yuko nyumbani lazima kuwe kunapikwa chakula.

Kuna baadhi ya nyumba ambazo hakupikwi ni watu wa kula barabarani tu. Ili nyumba yoyote ile igeuke kuwa nyumbani ni muhimu sana kuwe na chakula kila wakati, yaani jiko linapotumika kuandaa vyakula na harufu yake nzuri inaifanya kuwa na uhai wa kuitwa nyumbani.

Hata wanaoishi katika nyumba hiyo lazima wajisikie fahari kuishi humo na pia kukumbuka na kupenda kuwapo nyumbani muda wote.

# KATUNI




*KINYUNYIZO CHA LEO...

...UNAYEMBEBA NI HIYARI YAKE KUTHAMINI MGONGO WAKO

# IBADA YA KRISMASI PICHANI



Baadhi ya waumini wa KKKT wakishiriki ibada ya sikukuu ya Krismasi iliyofanyika Usharika wa Dodoma Mjini jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**



Askofu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) Dayosisi ya Dodoma, Amon Kinyunyu, akihubiri kwenye ibada ya Krismasi iliyofanyika Kanisa Kuu Usharika wa Dodoma Mjini jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**



Waumini wa KKKT Usharika wa Muheza mkoani Tanga wakiwa katika ibada ya Sikukuu ya Krismasi jana. Ibada hiyo iliendeshwa na Mchungaji Jonathan Mwamboza. **PICHA. NA STEVEN WILLIAM**



Watawa na waumini wakifuatilia mahubiri ya Askofu Augustino Shayo wa Kanisa Katoliki Jimbo la Zanzibar (hayuko pichani) kwenye mkesha wa Krismasi juzi. **PICHA: MARTIN KABEMBA**



Askofu Liberatus Sangu wa Kanisa la Katoliki Jimbo la Shinyanga, akibariki waumini wa kanisa hilo juzi, alipokuwa akiingia kanisani kuendesha misa ya mkesha wa Sikukuu ya Krismasi katika Kanisa Kuu la Mama Mwenye Huruma, Parokia ya Ngokolo mjini Shinyanga.



Kwaya Kuu ya Kanisa la Anglikana Dayosisi ya Dodoma wakiimba kwenye ibada ya Krismasi iliyofanyika Dodoma jana. **PICHA: PETER MKWAVILA .**

## MAKALA

# UTAMADUNI HUU UTALIANGAMIZA TAIFA



Na Magabilo Masambu

KUELEKEA mwishoni mwa mwaka 2021, niseme machache yaliyojitokeza miaka michache ambayo tusipoyasema yatajenga utamaduni wa kudumu siku zijazo. Kwa kawaida utamaduni huanza kujengeka taratibu pale tabia fulani zinapoanza kujitokeza. Zikiwa tabia njema basi hujenga utamaduni mzuri katika jamii lakini zikiwa mbaya hujenga utamaduni mbaya vilevile katika jamii.

Kwa utamaduni wetu wa kiafrika hasa wa kitanzania toka zamani, tumekuwa na utaratibu wa kuheshimiana lakini zaidi kuheshimu mawazo na maoni ya wale waliotutangulia kiumri au kimamlaka. Nakubali kwamba kutangulia huko hakuwezi kumfanya mtu akawa sahihi kwa kila jambo lakini angalau kwa uzoefu wa kuona na kujifunza mengi ama katika madaraka au maisha ya kawaida. Waswahili wanasema kuishi kwingi kuona mengi.

Kumekuwa na tabia ya baadhi ya viongozi hasa vijana kujitokeza waziwazi kuwakemea viongozi wastaafu au kutoa matamko yenye kuwatisha wasitumie uhuru wao wa kikatiba kutoa maoni kuhusu mambo mazito yanayoihusu nchi huku wakimwaga sifa kedekede kwa viongozi walioko madarakani.

Uhakika nilio nao ni kwamba wanaokusifu leo ukiwa na madaraka ya kuwateua kwenye nafasi mbalimbali ndiyo hao hao watakaokukemea utakapoyakosa madaraka hayo. Jambo moja muhimu ni kuwa makini sana na watu wanaokusifu sana leo na kuwakemea wengine kesho ama watakutukana au kukwambia umepitwa na wakati. Kutokana na ukweli huo, ukae kimya kama ambavyo tumewahi kusikia kauli kama hizo kutoka kwa baadhi ya viongozi vijana kwa umri lakini pia kwa uzoefu katika eneo la uongozi na siasa.

Jambo hili ni sawa kabisa na suala la kufuga joka nyumbani mwako ambalo kila siku unalipatia chakula siku likikosa ama litakutafuna mwenyewe au wanao. Hivyo ni muhimu kuwa makini na watu wa sampuli hiyo na hasa wanaokwambia tuko nyuma yako kuna siku utageuka hutawaona. Tukiwafurahia leo wanapojaribu kuwakemea wazee wetu kesho tukistaafu wembe ni ule ule tutakemewa na sisi.

Taifa lisiloheshimu mawazo ya wazee waliotangulia katika nafasi mbalimbali, litakosa mwelekeo mzuri kwa sababu ni vigumu sana kupata historia iliyo hai si ya kusoma kwenye vitabu. Tumefika mahali baadhi ya wazee wastaafu kwenye nafasi mbalimbali wamekuwa na hofu ya kutoa maoni yao, wakati mwingine wanalazimika kukanusha yale wanayoyasema kwa hofu tu kwamba wataonekana wasaliti badala yake wanaamua kukaa kimya na pale yanapotokea matatizo ambayo yangeweza kutatuliwa na ushauri wao, wanaishia kusema tulijua! Viongozi wote wenye nafasi mbalimbali lazima tufahamu kwamba hizi nafasi tulizo nazo si za kwanza kwetu. Walishakuwapo watu kama sisi wakapita, hivyo pamoja na mapya tunayoyataka yafanyike ni muhimu sana kurejea yaliyopita ili kuona wenzetu walifanikiwa au kushindwa wapi ili kufanya maboresho yenye tija kwa taifa. Hayo hayatawezekana kama tutaendelea kuwafanya waliopita washindwe kutoa ushauri wao waziwazi.

Miaka ile hasa katika awamu ya pili ya mzee wetu Mwinyi, Mwalimu Julius Nyerere akiwa tayari amekwishastaafu na yuko Butiama, alipokuwa anaona kuna jambo fulani halijakaa sawa, alikuwa anajitokeza waziwazi kusema hili hapana wakati mwingine aliendewa kuulizwa mzee hapa tunafanyaje? Utaratibu huo nadhani aliendelea nao mpaka mwisho wa maisha yake hapa duniani.

Wakati mwingine inaweza kuonekana kwamba wastaafu hawa wanaingilia masuala ambayo wao walishindwa kuyafanya. Bado huo hauwezi kuwa utetezi wa kupata fursa ya kutoa maoni yao kwa sababu inawezekana wakati wao changamoto wanazoziona leo hazikuwepo. Wengine wanasema kama wanataka kutoa maoni upo utaratibu. Nakubaliana nalo lakini si kila maoni yafuate utaratibu huo na hiyo itakuwa janja ya kuwapora uhuru wao wa kikatiba.

Tatizo linaweza kuwa si la wazee hawa pengine wanasubiri sana kuonwa kwa ajili ya ushauri hawaonwi. Namaanisha wazee wengi hupenda kufuatwa kuulizwa kwa baadhi ya mambo lakini nafikiri waulizaji hatuendi kuwauliza badala yake tunajifanyia tu mambo yetu kwa kuamini kwamba tunazo akili nyingi na uzoefu wa kutosha jambo ambalo binafsi naona si kweli. Kwa hiyo wanapoona mambo ambayo wanafikiri wangeulizwa na hawajaulizwa wanaamua kuyasema hadharani.

Nadhani tukiwapa fursa si tu wazee wastaafu bali kila mtu akiwa na nafasi sawa katika utoaji wa maoni namna ambavyo sisi kama nchi tunataka kujiendesha mambo mengi maovu yataepukika. Jambo hili pia halitafanikiwa ikiwa hatutajiona kama ndugu na kwamba taifa letu ni moja na makusudi ya kila mtu ni kuhakikisha Tanzania inaendelea kuwa nchi yenye sifa njema duniani.

Mambo haya lazima tuyatafakari sana. Kama taifa inawezekana pameanza kuwa na tatizo kubwa kuanzia kwenye familia zetu tabia ya kutowahesimu wazee wetu. Kuna wakati unasikiliza matamko mbalimbali ya baadhi ya viongozi unajiuliza hawa nao wana wazazi au wazee nyumbani kweli au wanafanya haya ili wale waliowapa nafasi hizi wafurahi? Unajiuliza tena hawa wanaosikiliza haya wanafurahi kweli na kama hawapendezwi mbona hawachukui hatua?

Nyumba yenye wazee ni nyumba yenye baraka sana. Waliofanikiwa kuishi na wazee wao watakuwa wanaelewa. Kuna wakati wakiwapo huwa umuhimu wao hauonekani sana lakini wanapoondoka ndipo unajua kwamba umekosa jambo muhimu sana.

**Jambo hili ndilo huwa linafanya watu wengi kuyapamba makaburi kwa vigae vyenye thamani. Tusisubiri kuweka picha zao kwenye kuta za majumbani mwetu na kuzihifadhi vizuri bali tuwaheshimu na kuthamini michango yao wakiwa wangali hai ili kuipa nafuu mioyo yetu pindi tunapowakosa.**

**0689157789**

## BURUDANI ILIYOTIKISA ENZI HIZO

# Vijana, Watoto zamani walivyoinjoi Krismasi



Na Adam Fungamwango

JANA waumini wa Kikristo duniani kote, waliungana na wenzao kusherehekea sikukuu ya Krismasi, ambayo kwa jina lingine huitwa Noeli.

Ni sikukuu inayosherehekewa Desemba 25 ya kila mwaka kuadhimisha kuzaliwa kwa Masiya, Yesu Kristo zaidi ya miaka 2000 iliyopita kwenye mji ya Bethlehemu.

Wakati wakubwa hupenda kwenda sehemu zenye vinywaji, nyama choma na burudani ya muziki, watoto wao hupenda kwenda sehemu kama vile baharini 'bichi' au maeneo yaliyotengwa kwa ajili yao kama vile kubembea na kuendesha farasi wa umeme.

Haya ni kwa wazazi na watoto wa kisasa. Miaka ya nyuma, maandalizi ya sikukuu hii yalikuwa tofauti. Yalikuwa makubwa zaidi na yaliyochukua muda mrefu kuliko sasa. Yalikuwa na pilikapilika nyingi kuliko sasa kwa wazazi na watoto pia. Siku hizi baba anaweza kupata pesa na kununulia watoto nguo wakati mwingine bila hata wao kujua. Wanashtukia zimeletwa tu. Kutokana na teknolojia kuwa ndogo, uhaba wa bidhaa kama nguo, viatu na vitu vingine vilisababisha kuwe na pilikapilika za aina yake. Kwanza kabisa watoto wa siku hizo wana nguo nyingi nzuri kiasi kwamba hata akinunuliwa mpya, zinakuwa hazina sana tofauti na alizonazo.

Zamani kwenye sikukuu kama hii picha linaanza kwanza kwenye redio. Hakukuwa na redio yoyote zaidi ya Radio Tanzania Dar es Salaam (RTD). Nyimbo za Krismasi zikianza kupigwa tangu tarehe 15, wote mtasikiliza na kila mtu atajua sikukuu inakuja, hivyo inaleta msisimko mno, tofauti na sasa ambapo kuna baadhi ya vituo ambavyo hawa havilazimiki kupiga nyimbo hizo.

Pia watoto na vijana wa sasa si wasikilizaji sana wa redio, zaidi ya televisheni na simu za mkononi ambapo husikiliza nyimbo wanazozitaka wao tu.

Kwa miaka ya karibuni hata miti halisi ya kupamba Krismasi haipo, badala yake ipo ya kutengenezwa ambayo si halisi. Hii imekuja kuua sana biashara ya miti halisi. Siku chache kabla ya Krismasi, baba atawapeleka kwa fundi cherehani kupima suruali, au gauni, wakati huo tayari vitambaa vimeshanunuliwa hasa wale wa vijijini. Wengine hupelekwa mjini kununuliwa gauni, shati, suruali na viatu.

Wazazi wakati huo walilazimika kuwachukua watoto wao kwenda nao mjini kwa sababu ya kujaribu nguo na viatu kwani isingewezekana kurudisha au kuanza kuirekebisha kwa fundi. Kulikuwa na maduka maalumu ya kununua nguo si kwa machinga kama sasa, lakini viatu hasa vya sikukuu na shule vilikuwa vinanunuliwa kwenye kampuni ya viatu ya Bora.

Na kama mtoto hatochukuliwa kupelekwa mjini kununuliwa viatu, basi litachukuliwa katarasi gumu au boksi, atalikanyaga, huku kalamu ikizungushwa kwa kuchorwa kuzunguka mguu, ili atakapoenda mjini basi viatu vitakachowekwa na kuwa sawa na mzunguko huo ulioko kwenye boksi au karatasi ngumu, vitakuwa vinamtosha mhusika na kweli ilikuwa hivyo.

Ilikuwa wiki ngumu kwa watoto wa zamani kuelekea kwenye sikukuu. Tena usiombee nguo zinunuliwe mapema. Ni kwamba kila mara atakuwa anakwenda kufungua sanduku na kuziangalia. Wakati mwingine atazijaribu na kuzirudisha akiombea sikukuu ifike upesi, avae akawaringishie wenzake ambao ana uhakika nao watakuwa na nguo mpya pia. Hapo sasa ni mashindano ya nani kapendeza zaidi ya mwingine.

Ukweli ni kwamba wazazi wa sasa wako karibu zaidi na familia zao hasa siku za sikukukuu mtu anaweza kutoka yeye mkewe na watoto, wakaenda popote pale kwa ajili ya kusherhekea, tofauti na zamani ambapo baba hakuwa na muda wa eti kuondoka akiwa ameongozana na watoto wake.

Kinababa wa enzi hizo wao walikuwa wanakwenda kivyao, kwenda kukutana wenyewe wanaume sehemu zao za burudani, hakuna mtoto yoyote anayetakiwa hapo. Kinamama nao walikwenda sehemu zao wakiwa na watoto wenye umri mtoto mchanga hadi miaka sita, na wale kuanzia miaka saba hadi 18 nao hawakutaka kuongozana na watoto, baba au mama. Hawa nao walikwenda sehemu zao. Hawa ndiyo asilimia kubwa ndiyo waenda 'bichi' au kule vijijini 'pikniki'.

Kwa miaka ya hivi karibuni pia kumekuwa na upungufu mkubwa wa maeneo ya watoto kwenda kusherehekea sikukuu kuliko wakubwa. Baa, hoteli, kumbi za burudani kwa wakubwa zimejaa tele, lakini watoto wamesahaulika. Hakuna maeneo ya wazi kama zamani yalikuwa yakimilikiwa na Jiji yenye bustani ambayo yatawafanya watoto kwenda kufurahia sikukuu. Kuna maeneo machache sana yaliyobaki baada ya mengi kupigwa bei, ambayo watoto hukusanyika na kupata burudani.

Zamani kulikuwa na meneo mengi ya wazi ambayo yalitengenezwa kama vizimba kwa kutumia magunia, na wakawa wanaingia na pesa, humo wanakuta ngoma za asili, maigizo, na michezo mbalimbali ya watoto kama kubembea, huku kukiwa pia na vyakula mbalimbali kama mishikaki, mihogo, Ice Cream na vingine vingi ambavyo watoto walifurahia sana.

Kukosekana maeneo ya burudani kwa watoto kumesababisha miaka ya hivi karibuni watoto nao kutinga kwenye kumbi za starehe. Licha ya kwamba hawaendi kustarehe, wanatumia majengo hayo ambayo kiafya kwao si mazuri. Wanakuwa wengi na kunakuwa na joto kali, hivyo wakati mwingine yanatokea matatizo makubwa. Kwenye miaka ya karibuni kumetokea maafa watoto walifariki kwenye ukumbi uliokuwa na joto.

Hii imesababisha hata Makamanda wa Polisi wa Mikoani kila mwaka kupiga marufuku 'disco toto', au watoto kuingia kwenye kumbi.

Ni kweli, ni hatari kubwa watoto kuingia kwenye kumbi ambazo zimefunikwa juu, lakini hili lingeepukika kama nchi ingekuwa na maeneo mengi ya wazi kama zamani kwa ajili ya watoto nao kuinjoi sikukuu kama wenzao wa zamani.

# HADITHI

TINA, msichana kutoka Mpanda, mkoani Katavi anafiwa na wazazi wake wote wawili kwa ajali ya gari akiwa na miaka 10 tu. Tabu alizozipata kutokana na kunyanyaswa na ndugu zake, zilimfanya kuishi maisha ya mateso. Hata shule aliishia la saba tu. Alipofikisha umri wa miaka 18 akakimbilia Dar es Salaam na kuanza kufanya kazi za ndani. Baadaye akabahatika kupata kazi za ndani kwa mfanyabiashara mmoja maarufu, Hafidh Chilambo. Mfanyabiashara huyo anafariki kwa kula chakula kilichowekwa sumu. Chakula hicho kilipikwa na Tina. Mahakama Kuu inamhukumu adhabu ya kunyongwa hadi kufa. Je ni wafanyabiashara wenzake Chilambo ndiyo waliomtuma msichana huyo kwa kumwahidi mamilioni ya pesa kutokana na ugomvi wa kibiashara? Au ni kwa sababu hajalipwa mshahara wake wa miezi sita aliokuwa anadai? Fuatilia kila nakala ya Nipashe ili kuupata ukweli ulio nyuma ya pazia wa sakata hili.

# Ajenda ya siri-10

**Na Adam Fungamwango**
**(0716 350534)**

EDDY alikaa kwenye gogo la mnazi. Akaingiza mfukoni na kutoa noti ya Shilingi elfu kumi.

"Najua nitakupotezea dakika kadhaa, kwa hiyo nafidia muda wako, utapata soda baadaye." Alisema huku akimpa noti moja ya thamani ya pesa hiyo.

Mzee aliendelea kushangaa, lakini aliipokea na kuiweka kwenye mfuko wa koti lake. Kwake ilikuwa ni pesa nyingi sana ambayo hakufikiria kuipata ghafla na bila sababu yoyote siku ile.

Sasa alionekana kuchangamka. "Mimi naitwa mzee Mwayangu, kote huku najulikana, hakuna ambaye hanifahamu, na nyumba yangu haiko mbali sana na hapa, wewe mwenzangu unatokea wapi?"

"Mzee mimi natoka mbali sana, kwanza samahani, maana maswali yangu unaweza ukayaona kama ya kipuuzi hivi."

"Maswali gani hayo?"

"Kwanza mimi ni mjomba wa msichana mmoja anaitwa Tina, ambaye kama una kumbukumbu vizuri alihukumiwa kunyongwa hadi kufa kutokana na kumuua tajiri yake."

"Huyu jamaa wa pale mbele aliyewekewa sumu kwenye chakula?"

"Ndiyo huyo huyo mzee."

"Duh, pole sana, wewe ndiye mjomba wake?"

"Ndiyo." Alijibu na moja kwa moja akaanza kuingiza maswali aliyotaka kumuuliza.

"Hivi mpwa wangu unamfahamu?"

"Haa, yule msichana, si alikuwa anapita hapa tena namtania mchumba wangu. Hawezi kupita hapa bila kunisalimia. Tena akipita hapa alikuwa ujue anakwenda duka la dawa hapo."

"Ina maana mzee kumbe si mara ya kwanza kununua dawa kwenye duka lile?"

"Yaani ndiyo duka lake. Hata yeye mwenyewe akiumwa, ananiambia babu leo kichwa kinauma, nakwenda kununua dawa. Pole sana kwa yaliyompata mpwao, sasa unachohitaji hapo ni nini? Kwenda kule kwa tajiri yake?"

"Ndiyo, kuna vitu ameviacha kule vya muhimu sana, lakini kabla sijakwenda ni lazima nijue nakwenda vipi, nisije nikafukuzwa au kugeuziwa kibao na familia ya marehemu."




**"Ndiyo, kuna vitu ameviacha kule vya muhimu sana, lakini kabla sijakwenda ni lazima nijue nakwenda vipi, nisije nikafukuzwa au kugeuziwa kibao na familia ya marehemu."**

"Kweli kabisa kijana, ila mimi nitakusaidia kama unataka kwenda."

"Nitashukuru, ila napenda kufahamu, siku ya mwisho kupita hapa ulimuona?"

"Kijana, mimi nipo hapa hapa, nikitoka naenda msalani, chakula wajukuu wangu huwa wananiletea. Nafungua kibanda changu saa mbili, nafunga saa tatu usiku kila siku. Nilimuona na tuliongea."

"Alikwambia nini?"

"Nilisalimianana naye, akaenda kwenye duka la dawa, aliporudi nilimuuliza unaumwa? Akanijibu hapana, dawa hizi siyo zangu. Za nani? Hakunijibu, alionekana kuwa na haraka."

"Wala hakusema nani anaumwa au ametumwa na nani?"

"Wala, ila alipokuwa anaondoka, mbele kule nilimuona amesimama kwenye mlango wa gari, halafu likaondoka na yeye akawa anaendelea na safari zake, nikaona yule tayari ameshakuwa msichana mkubwa sasa, inawezekana amesimamishwa na mwanaume mwenye gari wanaongea, si unajua tena vijana."

Alichofikiria Eddy kilikuwa sahihi, siku alipomuona alipopita na Mwahija alijua huenda mzee huyo akawa kuna kitu angalau kidogo ambacho atakuwa anakifahamu kuhusiana na suala hilo, kwani alijua wazee wa mjini wanajua mengi na wanaambiwa mengi, pia hawataki kitu chochote kiwapite. Pia kutokana na kuwa yupo karibu na duka la dawa, huenda anaweza akawa anafahamu kitu chochote kuhusu Tina, au kuambiwa kuwa alikwenda kununua dawa sehemu hiyo ambayo ndiyo iliyoleta maafa. Na kweli kumbe alikuwa anajua baadhi ya vitu. Ndiyo maana aliamua kumfuata siku aliyotenga mwenyewe.

************************************

Hatua kadhaa alizopiga baada ya kutoka kwa mzee Mwayangu, alikwenda moja kwa moja hadi sehemu ambayo aliyodai Tina alisimamishwa na mwanaume mmoja ambaye alikuwa kwenye gari.

Ni siku hiyo ambayo inasadikika ndiyo aliyotoka kununua dawa zilizogeuka sumu na kumuua Chilambo, kwani siku mbili baadaye alikamatwa.

Kulikuwa na kona, na mkabala wake kulikuwa na flemu ambayo ilikuwa imepambwa na picha za mastaa wa bongo movie na wa filamu za nje ya nchi.

Wala haikupi shida kujua kuwa ni sehemu inayouzwa au kukodishwa filamu na tamthilia za nje na za Bongo.

Alisongea hadi kwenye kwenye mlango na kumkuta kijana anayeonekana na umri kati ya miaka 20 au 22 hivi.

"Hujambo kijana."

"Sijambo karibu braza."

"Ahsante sana."

"Vipi unahitaji picha?"

"Hapana, mimi siyo mteja wa kununua au kukodisha picha."

"Enhee, unahitaji nini nikusaidie?"

"Naomba kumuuliza dada mmoja anaitwa Tina."

"Tina gani?"

"Tina, msichana mmoja aliniambia anafanya kazi maeneo haya jirani, anafanya kazi za ndani tu."

"Du, ni nani yako?"

"Ni mpenzi wangu, aliniambia anaishi maeneo haya haya ya jirani." Eddy alidanganya. Hakutaka kusema ni ndugu yake kwa sababu ingemtia wasiwasi kuwa kama ni ndugu anashindwaje kujua kama amehukumiwa?

"Mara ya mwisho kukutana naye ni lini?"

"Miezi saba iliyopita sasa."

"Braza we kiboko, binti mdogo kama yule, si ungetuachia sisi tu."

"Kwanza ujue tayari ana miaka 18, hasomi, halafu nyinyi vijana kama wewe mna mambo mengi, hamjui kujali, leo ukiona huyu mzuri, kesho unamuona mwingine barabarani, unamuacha." Eddy alizidi kumpigisha hadithi kijana huyo kwa lengo la kumlainisha ili kama kuna analolijua kuhusu Tina.

"Kwani wewe unaishi wapi, hapa hapa nchini?"

"Hapana, nimetoka Afrika Kusini siku tatu zilizopita."

"Pole sana mpenzi wangu amehukumiwa kunyongwa." Alisema kijana yule na hapo hapo Eddy akaigiza kupatwa mshtuko mkali na hakuonekana kusema kitu chochote, mpaka alipokaribishwa kwenye benchi akae ili asije kuanguka."Kwani ilikuwaje?" Aliuliza akijifanya hajui chochote kile. Kijana yule aliyejitambulisha kwa jina la Nanje, alimsimulia mwanzo hadi mwisho. Ilikuwa ni yale yale tu yanayojulikana.

"Wewe unadhani ni kweli alimuua bosi wake?"

"Siamini." Lilikuwa ni jibu lilolomshtua Eddy. Na moja kati ya jibu alililoliona la maana na alilolohitaji ni hilo. "Kwa nini unadhani si kweli?"

"Sikiliza nikwambie." Alianza kuongea kwa sauti ndogo na kuonekana kuwa na wasiwasi, akiangalia huku na huko kama watu wapo karibu.

**ITAENDELEA JUMAPILI**



# MENINA AJIITA 'MALKIA' ATANGAZA VITA RASMI

MWIGIZAJI wa filamu za Bongo Muvi, Menina, ameamua kuingia rasmi katika muziki na kueleza anataka kurekebisha mambo baada ya kuona tasnia hiyo inayumba.

Menina ameingia akiwa na EP yake inayoitwa 'The Queen Is Back'ambayo ina nyimbo nne.

"Katika muziki hakuna Malkia na mimi nimejiona nafaa kuwa katika nafasi hiyo na ndio maana nimekuja kuweka sawa baada ya kuona muziki unayumba hasa kwa wanawake," amesema Menina.

## Card B kutoa Bil 4 kawaida sana

MASTAA wa Bongo wakitoa zawadi hata ndogo itasambazwa kila kona dunia ifahamu kwamba hata yeye ana uwezo, lakini kwa rapa wa Marekani, Cardi B ameonekana hataki misifa kwani licha ya zawadi yake ya kufa mtu, lakini hana habari na mtu.

Hivi karibuni Card B alimwagia mume wake Offset, kiasi cha dola milioni 2, sawa na shilingi bilioni 4 kama zawadi.

Cardi B amempa mume wake hundi akiwa jukwaani katika ukumbi mmoja wa starehe, huku akionekana hana wasiwasi kwa kufanya tukio hilo hadharani.

Imekuwa utaratibu wa wawili hao kupeana zawadi na kufanyiana 'sapraizi' kwenye siku za kuzaliwa kwao.



## DIAMOND, ZUCHU lisemwalo lipo, iko siku watajua

BADO uvumi kwamba Diamond anakamilisha mipango ya kumuoa msanii wake Zuchu, unazidi kusambaa kwa kasi licha ya dada wa mwanamuziki huyo kujaribu kupuuza.

Katika mitandao ya kijamii, baadhi ya watu wanajadili endapo Diamond ataamua kufunga ndoa na Zuchu, kama wataweza kudumu kutokana na tabia yake ya kuwa na wanawake wengi.

Mpaka sasa Diamond amejihusisha kimapenzi na mastaa wa kike zaidi ya watano na kufanikiwa kuwa na watoto wanne.

Hivi karibuni dada yake, Esma aliulizwa na mmoja wa wafuasi wake kwenye Instagram kuhusu uvumi huo, lakini alisema taarifa hiyo hana na ndiyo kwanza anasikia.

Esma amesema kitu hicho hakipo pamoja na kwamba kumekuwa na madai ya Diamond na Zuchu kutoka kimapenzi siku nyingi.



# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### GUARDIOLA AMTAKA HAALAND

KOCHA wa Manchester City, Pep Guardiola amesema atahifadhi fedha alizomuuza, Ferran Torres, 21, ambaye anajiandaa kujiunga na Barcelona kwa pauni milioni 55, ili zitumike kumsajili mshambuliaji Borussia Dortmund na Norway, Erling Braut Haaland (21). ***(Manchester Evening News)***

### YAMKATAA MARTIAL

NEWCASTLE United haitamshawishi fowadi wa Manchester United na Timu ya Taifa ya Ufaransa, Anthony Martial, 26, kujiunga nao, kwa sababu itawagharimu pauni milioni sita. ***(Football Insider)***

### EN-NESYRI ANUKIA ARSENAL

ARSENAL imemtambua straika wa Sevilla, Youssef En-Nesyri, 24 kama chaguo lao la usajili. ***(Express)***

### SPURS KUMWACHIA DELLE

TOTTENHAM Hotspur ipo tayari kumwachia kiungo wa Timu ya Taifa ya England, Dele Alli, 25, kuondoka kwa mkopo ifikapo Januari. ***(Evening Standard)***

### DEMBELE MITANO TENA

WINGA wa Timu ya Taifa ya Ufaransa, Ousmane Dembele, 24, amekubali kusaini mkataba mpya na Barcelona wa miaka mitano. Mchakato huo utafanyika mapema wiki ijayo. ***(Sport)***

### ROMA KUIBOMOA ARSENAL

AS Roma ipo kwenye mazungumzo ya kutaka kumsajili kiungo wa Arsenal na Timu ya Taifa ya England, Ainsley Maitland-Niles, 24 kwa mkopo Januari. ***(ESPN)***

### PHILLIPS AIKATAA UNITED

KIUNGO wa England, Kalvin Phillips, 26, anahusishwa na uhamisho wa kwenda Manchester United, ambapo yeye mwenyewe anataka kurefusha mkataba wake na Leeds United. ***(Mail)***

### DIKE AGOMBEWA ENGLAND

STRAIKA wa Orlando City na Marekani, Daryl Dike, 21, anawaniwa na klabu nyingi za Uingereza, zikiwamo West Ham, Newcastle, Brighton, Leeds na West Brom. ***(Team Talk)***

### TRIPPIER KITAELEWEKA

ATLETICO Madrid inatarajia kupokea ofa kwa ajili ya mlinzi wa kulia, raia wa England, Kieran Trippier, 31, kutoka Newcastle United Januari. ***(ESPN)***

### NKETIAH AGEUKA LULU

KLABU za West Ham, Crystal Palace na Brighton zipo kwenye mbio moja za kumwania straika wa Arsenal, Eddie Nketiah, 22. ***(Mail)***

### LENGLET: SIONDOKI BARCA

MLINZI wa Timu ya Taifa ya Ufaransa, Clement Lenglet, 26, anataka kubakia Barcelona, licha ya kukosa nafasi ya kuanza msimu huu. ***(Marca)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# ARTETA AFUNGUKA ANACHOTAKA ARSENAL

**Kocha huyo asema anataka kuona nidhamu, heshima na hali ya kujitolea...**

**LONDON,** England

KOCHA wa Arsenal, Mikel Arteta, ameweka wazi kitu anachohitaji kutoka kwa wachezaji wake, wakati akisisitiza nidhamu na kujituma ni moja ya vitu anavyozingatia.

**Arteta amesema haiendeshi klabu ya Arsenal kidikteta kama wengi wanavyodhani, lakini anataka heshima, nidhamu na kujitolea kutoka kwa wachezaji wake.**

Taarifa hizo zimekuja baada ya Arteta kumwondoa katika kikosi mshambuliaji Pierre-Emerick Aubameyang na baadaye kumvua unahodha wa timu hiyo kutokana na utovu wa nidhamu.

Aubameyang hajacheza mechi nne katika mwezi huu wala kushiriki katika mazoezi na kikosi cha kwanza kutokana na ishu za kinidhamu baada ya kuchelewa kurudi kambini.

Kocha huyo raia wa Hispania ameweka wazi ni bora kuondoka ndani ya klabu hiyo endapo atashindwa kupata vitu anavyovitaka kutoka kwa wachezaji wake ambavyo ni nidhamu na kujitolea.

"Sipo hapa kwa ajili ya kumwonea mchezaji yoyote, tunachozingatia ni misingi ya klabu nayo ni nidhamu na heshima," amesema Arteta akinukuliwa na BBC Sport.

"Mchezaji kazi yake ni kucheza mpira na kuisaidia timu, lakini sio sehemu ya kujionyesha wewe ni mkubwa zaidi kuliko wengine, katika hilo lazima nizingatie nidhamu na heshima."









# SIMEONE AWAPA LIKIZO YA MASHARTI WACHEZAJI

**MADRID,** Hispania

DIEGO Simeone amedhamiria kubadilisha mambo katika klabu ya Atletico Madrid baada ya kujikuta wapo kwenye kiwango kibaya msimu huu.

Atletico Madrid walitarajiwa kutetea vyema ubingwa wao wa Ligi Kuu Hispania, LaLiga, wakiwa na kikosi cha timu chenye ubora wa hali ya juu.

Lakini wameingia mapumziko ya Krismasi chini ya pointi 17 nyuma ya vinara wa ligi hiyo Real Madrid baada ya kupoteza mechi nne mfululizo. Los Rojiblancos hao wamepoteza mbele ya Mallorca, Atletico Bilbao, Real Madrid na Granada hivi karibuni.

Huku kukiwa na nafasi ndogo ya kushinda Ligi ya Mabingwa Ulaya, msimu wa Atletico unaweza kumalizika kwa upande wa kuwania mataji msimu huu, huku Copa del Rey pekee ikionekana kuwa kwenye unafuu zaidi kwao kwa wakati huu.

Wakati presha inazidi kupanda, Simeone amewaambia wachezaji wake mambo matatu ambayo wanapaswa kufanya ili kubadilisha mwelekeo wakiwa kwenye mapumziko ya Krismasi. Baada ya kushindwa kwa Granada, Diego Simeone alisema ni wakati wa wachezaji wake: "Kuburudisha akili, kustarehe na kufanya kazi."



# Pele atoka hospitali, hali yake bado tete

**SAO PAULO,** Brazil

GWIJI wa soka wa Brazil, Edson Arantes do Nascimento "Pele" aliruhusiwa kutoka hospitali juzi ambako alikuwa amelazwa kwa wiki kadhaa kutokana na kusumbuliwa na maradhi ya utumbo.

Pele alilazwa katika hospitali ya Albert Einstein tangu Desemba 9, mwaka huu ili kupokea "kipindi cha mwisho cha matibabu ya kemikali" baada ya matatizo aliyokuwa nayo kufuatia kugunduliwa kwa saratani na uvimbe wake ulitolewa Septemba 4, mwaka huu katika hospitali hiyo hiyo.

Pele mwenye umri wa miaka 81 aliondoka akitabasamu huku ripoti ya matibabu ikionyesha "yuko imara na ataendelea na matibabu ya uvimbe kwenye utumbo mpana uliotambuliwa Septemba, mwaka huu".

Taarifa ambazo zimetolewa kuhusu hali ya afya ya mchezaji huyo maarufu zimekuwa chache, kwani wakati wa upasuaji huo ugonjwa aliokuwa akiumwa haukuwekwa wazi.

Aliandika kwenye mitandao yake ya kijamii "Nitaitumia sikukuu ya Krismasi kuwa na familia yangu nyumbani."

## HABARI MICHEZO


# 4,667,160 JACKPOT MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 26/12/2021 | 18:00 | Hull City vs Blackburn | 2.99 | 3.18 | 2.32 |
| 02. 26/12/2021 | 18:00 | Lincoln vs MK Dons | 2.89 | 3.29 | 2.32 |
| 03. 26/12/2021 | 18:00 | Cheltenham vs Plymouth | 2.90 | 3.34 | 2.29 |
| 04. 26/12/2021 | 18:00 | Fleetwood Town vs Shrewsbury | 2.29 | 3.19 | 3.04 |
| 05. 26/12/2021 | 18:00 | Motherwell vs Livingston | 2.27 | 3.11 | 3.20 |
| 06. 26/12/2021 | 18:00 | Dundee Utd vs Hibernian | 3.30 | 3.11 | 2.22 |
| 07. 26/12/2021 | 18:00 | Kortrijk vs Royal Antwerp | 2.71 | 3.40 | 2.43 |
| 08. 26/12/2021 | 18:00 | Inverness vs Partick Thisle | 2.33 | 3.23 | 2.89 |
| 09. 26/12/2021 | 18:00 | Hamilton vs Kilmarnock | 3.11 | 3.26 | 2.19 |
| 10. 26/12/2021 | 18:00 | Ayr United vs Raith Rovers | 3.04 | 3.14 | 2.29 |
| 11. 26/12/2021 | 18:00 | Morton vs Queen of South | 2.56 | 3.30 | 2.56 |
| 12. 26/12/2021 | 18:00 | Albion Rovers vs Stranraer | 2.60 | 3.17 | 2.50 |
| 13. 26/12/2021 | 18:00 | Alfreton vs Boston Utd | 2.46 | 3.23 | 2.60 |


## MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

### JUMAPILI - 26 - DESEMBA 2021

| TAREHE | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:30 | 2106 | Caykur Rizespor vs Gaziantep BB | 2.66 | 3.31 | 2.52 |
| 15:30 | 2460 | St Johnstone vs Celtic | 9.86 | 5.52 | 1.26 |
| 15:30 | 4094 | Cercle Brugge vs Brugge | 4.04 | 3.75 | 1.78 |
| 16:00 | 4103 | Goeztepe vs Adana Demirspor | 2.40 | 3.25 | 2.85 |
| 16:00 | 5637 | Alanyaspor vs Fatih Karagumruk | 2.15 | 3.41 | 3.16 |
| 17:00 | 4700 | Kerala Blasters FC vs Jamshedpur | 2.51 | 3.23 | 2.55 |
| 17:30 | 2354 | Al Salmiyah vs AL Qadsia | 3.47 | 3.66 | 1.86 |
| 18:00 | 1688 | Rangers vs St Mirren | 1.11 | 7.89 | 19.72 |
| 18:00 | 1838 | Luton Town vs Bristol City | 1.67 | 3.68 | 4.80 |
| 18:00 | 2023 | Huddersfield vs Blackpool | 2.13 | 3.27 | 3.27 |
| 18:00 | 2061 | Dunfermline vs Arbroath | 3.03 | 3.28 | 2.22 |
| 18:00 | 2113 | Accrington vs Rotherham | 4.42 | 3.68 | 1.72 |
| 18:00 | 2205 | Falkirk FC vs Clyde | 1.81 | 3.55 | 3.99 |
| 18:00 | 2459 | Athletic Youssoufia vs Difaa El Jadidi | 2.57 | 3.05 | 2.61 |
| 18:00 | 2552 | Cheltenham vs Plymouth | 2.90 | 3.34 | 2.29 |
| 18:00 | 2697 | Ayr United vs Raith Rovers | 3.04 | 3.14 | 2.29 |
| 18:00 | 2804 | Kortrijk vs Royal Antwerp | 2.76 | 3.40 | 2.39 |
| 18:00 | 3053 | Fleetwood Town vs Shrewsbury | 2.29 | 3.19 | 3.04 |
| 18:00 | 3061 | Burnley vs Everton | 2.11 | 3.25 | 3.60 |
| 18:00 | 3125 | Cove Rangers vs East Fife | 1.36 | 4.80 | 7.05 |
| 18:00 | 3259 | Hearts vs Ross County | 1.56 | 4.04 | 5.31 |
| 18:00 | 3714 | Lincoln vs MK Dons | 2.89 | 3.29 | 2.32 |
| 18:00 | 3859 | Morton vs Queen of South | 2.56 | 3.30 | 2.56 |
| 18:00 | 3930 | Manchester City vs Leicester | 1.21 | 6.49 | 12.30 |
| 18:00 | 3991 | Airdrieonians vs Alloa Athletic | 2.08 | 3.41 | 3.22 |
| 18:00 | 4275 | Dundee Utd vs Hibernian | 3.30 | 3.11 | 2.22 |
| 18:00 | 4282 | Standard Liege vs Zulte Waregem | 1.60 | 4.25 | 4.65 |
| 18:00 | 4773 | Norwich City vs Arsenal | 6.56 | 4.31 | 1.48 |
| 18:00 | 4797 | Hull City vs Blackburn | 2.99 | 3.18 | 2.32 |
| 18:00 | 4940 | Inverness vs Partick Thisle | 2.33 | 3.23 | 2.89 |
| 18:00 | 5021 | Aberdeen vs Dundee FC | 1.64 | 3.70 | 5.13 |
| 18:00 | 5096 | West Ham vs Southampton | 1.84 | 3.80 | 3.95 |
| 18:00 | 5127 | Hamilton vs Kilmarnock | 3.11 | 3.26 | 2.19 |
| 18:00 | 5424 | Tottenham vs Crystal Palace | 1.73 | 3.79 | 4.59 |
| 18:00 | 5495 | Middlesbrough vs Nottingham | 2.07 | 3.23 | 3.48 |
| 18:00 | 5801 | Motherwell vs Livingston | 2.27 | 3.11 | 3.20 |
| 18:00 | 5806 | Queens Park vs Dumbarton | 1.52 | 4.11 | 5.48 |
| 18:30 | 5493 | Al Sharjah SC vs Baniyas | 1.83 | 3.57 | 3.67 |
| 19:00 | 2149 | Fenerbahce vs Yeni Malatyaspor | 1.35 | 4.83 | 7.88 |
| 19:45 | 1212 | Al Ittihad Jeddah vs Al-Ettifaq | 1.74 | 3.77 | 4.37 |
| 19:45 | 5631 | Kazma SC vs Al Kuwait SC | 3.04 | 3.33 | 2.12 |
| 20:15 | 5703 | Olympique Safi vs Olympique Khouribga | 2.60 | 2.79 | 2.79 |
| 20:20 | 3933 | Bromley vs Southend | 1.74 | 3.82 | 4.01 |
| 20:30 | 3862 | Union Saint Gilloise vs KAA Gent | 2.17 | 3.50 | 3.05 |
| 20:30 | 5625 | Aston Villa vs Chelsea | 5.01 | 3.76 | 1.68 |
| 21:00 | 1068 | Hapoel Hadera vs Hapoel Beer Sheva | 4.81 | 3.66 | 1.62 |
| 21:00 | 1698 | Coca Cola vs Al Ahly Cairo | 6.08 | 4.42 | 1.46 |
| 21:30 | 1618 | Beitar Jerusalem vs Hapoel Katamon | 1.98 | 3.18 | 3.56 |
| 23:00 | 3385 | Oostende vs Racing Genk | 3.45 | 3.64 | 1.96 |
| 23:00 | 3399 | Brighton vs Brentford | 1.94 | 3.40 | 4.00 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# LIGI KUU YA WANAWAKE YAANZA NA MABAO KIBAO

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI msimu mpya wa 2021/22 wa Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania Bara ulianza Desemba 23, mwaka huu, jumla ya mabao 30 yamefungwa katika mechi sita za raundi ya kwanza zilizochezwa kwenye viwanja mbalimbali hapa nchini.

Ligi hiyo iliyoanza Alhamisi ilishuhudia mabingwa watetezi, Simba Queens ikiinyuka bila huruma Ruvuma Queens mabao 15-0 kwenye Uwanja wa Mo Arena na kuweka rekodi ya aina yake, huku mechi zote tano zilizofuata zikizaa tena mabao 15.

Siku hiyo hiyo, kwenye Uwanja wa Nyamagana jijini Mwanza wenyeji Alliance Girls walianza msimu mpya kwa ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Mlandizi Queens kutoka mkoani Pwani.

**Ligi hiyo iliendelea tena siku ya Ijumaa kwa washindi wa pili wa msimu uliopita, Yanga Princess kupata ushindi wa ugenini wa mabao 2-0 dhidi ya Baobab Queens, mechi ikichezwa kwenye Uwanja wa Jamhuri jijini Dodoma.**

Timu ya Fountain Gate Princess iliishikisha adabu Ilala Queens kwa kupata mabao 4-0, kwenye Uwanja wao wa nyumbani, wakati kwenye Uwanja wa Meja Isamuhyo, Maafande wa JKT Queens waliisasambua Oysterbay Girls mabao 3-1.

TSN Queens, ikiwa nyumbani kwenye Uwanja wa CCM Kirumba ilikiona cha moto pale ilipokubali kuchabangwa mabao 4-0 dhidi ya The Tigers Queens ya jijini Arusha.

Ukiondoa mabao ya mechi ya Simba dhidi ya Ruvuma Queens, idadi ya mabao ya mechi zote zilizofuata ni 15.

Kwa matokeo hayo, Simba Queens imeanza raundi ya kwanza tu ikiwa kileleni, ikiwa na pointi tatu na mabao 15, Fountain Gate Princess ikishika nafasi ya pili na The Tigers Queens ikiwa kwenye nafasi ya tatu huku JKT Queens ikikamata nafasi ya nne na Yanga Princess iko kwenye nafasi ya tano wakati Ruvuma Queens inaburuza mkia.

# *DTB, Gwambina mechi ya kibabe*

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa DTB FC, Ramadhani Nsanzurwimo, amesema ameandaa vyema kikosi chake ili kiibuke na ushindi kuelekea mchezo wa Ligi ya Championship dhidi ya Gwambina FC utakaochezwa leo kwenye Uwanja wa Gwambina ulioko Misungwi jijini Mwanza.

Akizungumza na gazeti hili jana, Nsanzurwimo alisema wachezaji wake wako tayari kwa mapambano na anaamini watatimiza kile alichowaelekeza kwa ajili ya kufikia malengo.

"Wachezaji wangu wote wako fiti kwa ajili ya kuhakikisha tunarejea Dar es Salaam na pointi sita ambazo tumekuja kuzitafuta katika Kanda ya Ziwa," alisema Nsanzurwimo.

Kocha huyo aliongeza wao kila mechi wanaiona ni sawa na fainali kwa sababu wanataka kuendelea kubakia kwenye uongozi katika msimamo wa ligi hiyo ambayo zamani ilijulikana kama Ligi Daraja la Kwanza.

Aliongeza anawaheshimu Gwambina FC na wanaingia uwanjani kwa tahadhari lakini wakipambana kwa dakika zote 90 na hatimaye wavune pointi tatu walizozifuata katika mchezo huo. Baada ya mechi ya leo, DTB FC itabakia Mwanza kwa ajili ya mchezo wao mwingine dhidi ya Pamba FC utakaochezwa Januari Mosi, mwakani kwenye Uwanja wa Nyamagana.



Winga wa Coastal Union, Abdul Suleiman 'Sopu' (kushoto), akipambana kuwania mpira dhidi ya mchezaji wa Mbeya City katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara iliyochezwa kwenye Uwanja wa CCM Mkwakwani jijini Tanga juzi. Coastal Union ilishinda mabao 3-2. **PICHA: MTANDAO**

Michezo
Jumapili Desemba 26, 2021
Nipashe



Arteta afunguka anachotaka Arsenal

UKURASA 21

# Yanga: Biashara hawaponi

**●●● Lakini yajipanga kucheza kwa tahadhari huku kipa Metacha...**

**Na Saada Akida**

TUNATAKA pointi tatu. Hiyo kauli imetolewa na timu mbili zinazokutana katika mechi ya Ligi Kuu ya NBC Tanzania Bara itakayowakutanisha wenyeji Yanga dhidi ya Biashara United leo kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam.

Hata hivyo, Biashara United leo itashuka dimbani ikimkosa Kocha wake Mkuu, Patrick Odhiambo, ambaye amerejea kwao Kenya baada ya kuwapo kwa sintofahamu kati yake na mabosi wa timu hiyo.

Akizungumza jana jijini, Kocha Mkuu wa Yanga, Nesreddine Nabi, alisema kikosi chake kimejiandaa vizuri kuelekea mchezo huo na kama mechi zilizopita, wamedhamiria kuondoka na pointi tatu.

Nabi alisema anahitaji kupata ushindi katika mechi hiyo ili kuendelea kujiimarisha kwenye kilele cha msimamo wa ligi hiyo ambayo inaonyesha ushindani kadri kila michezo inavyochezwa.

"Wachezaji wangu wanatakiwa kufuata maelekezo niliyowapa kama ilivyo katika michezo iliyopita ili kuhakikisha tunaendelea kuvuna matokeo mazuri katika mchezo huu, tutaingia uwanjani kama tunacheza fainali," alisema Nabi.

Kocha huyo alisema mechi zote za ligi ni ngumu na hasa katika mzunguko huu wa kwanza ambao kila timu inahitaji kufanya vyema kwa ajili ya kufikia malengo waliyojiwekea.

Mkurugenzi wa Ufundi wa Biashara United, Madenge Omari, alisema timu yao imejiandaa vizuri kuhakikisha wanapata pointi tatu muhimu za mchezo huo na kurejesha hali ya kujiamini kwenye kikosi chao.

Omari alisema wanatambua Yanga ni timu kubwa na yenye wachezaji wazuri lakini hata wao wamejiandaa vizuri kwa ajili ya kupata matokeo chanya ili kujiweka katika mazingira mazuri katika msimamo wa ligi.

"Tunawaheshimu Yanga na tutacheza kwa tahadhari kubwa, tumekuja kucheza soka kwa kuhakikisha hatupotezi mchezo huo kirahisi kama wanavyotuchukulia wapinzani wetu," alisema Omari.

Naye nahodha wa Biashara United, Abdulmajid Mangalo, alisema makocha wameshamaliza kazi yao na sasa kazi iliyobaki ni kwao wachezaji kuhakikisha wanaondoka na ushindi wa ugenini.

Yanga ndio vinara wa ligi hiyo wakiwa na pointi 23 huku kukiwa na tetesi za kumrejesha aliyekuwa golikipa wao, Metacha Mnata ambaye bado ana mkataba wa miaka miwili na waajiri wake wa sasa, Polisi Tanzania.

Taarifa za awali zilizopatikana jijini jana zinasema tayari Metacha amevunja mkataba na meneja wake, Jemedari Said, ambaye anatajwa kutokuwa na mahusiano mazuri na Yanga inayosaka kipa ili kubeba mikoba ya Djigui Diarra aliyeteuliwa kwenye kikosi cha Mali kwa ajili ya kushiriki fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON 2022).

Mechi nyingine ya ligi hiyo itakayochezwa leo itakuwa ni kati ya wenyeji Kagera Sugar dhidi ya Tanzania Prisons, kwenye Uwanja wa Kaitaba, Bukoba mkoani Kagera.



Kiungo mpya wa Yanga, Salum Abubakar 'Sureboy', ambaye ametangazwa rasmi kujiunga na klabu hiyo juzi. Sureboy ametua kwa vinara wa Ligi Kuu Bara akitokea Azam FC ambayo aliitumikia kwa muda wa miaka 10. **PICHA: YANGA SC**

## Ushindi waipa jeuri Simba SC

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI ripoti ya mapendekezo ya usajili wa dirisha dogo ikiwa imeshatua mezani kwa mabosi, Kocha Msaidizi wa Simba, Thierry Hitimana, amesema benchi la ufundi la timu hiyo limefurahishwa na kiwango kilichoonyeshwa na wachezaji katika mechi ya Ligi Kuu ya NBC Tanzania Bara dhidi ya KMC iliyochezwa juzi mkoani Tabora.

Simba, mabingwa watetezi wa ligi hiyo waliichapa KMC mabao 4-1 katika mchezo wa raundi ya tisa uliochezwa kwenye Uwanja wa Ali Hassan Mwinyi.

Hitimana aliliambia gazeti hili mabao mawili ya mapema waliyoyapata yalisababisha wachezaji kujiamini na kucheza soka safi, lakini baadaye walionekana kuishiwa nguvu kwa sababu bado afya zao hazijaimarika vyema kutokana na ugonjwa uliowapata.

"Tulifunga mabao mawili, ikatupatia kujiamini. Kwenye mechi hii hakukuwa na nafasi nyingi, lakini nafasi chache ambazo tumezipata tulizitumia, kama mtakumbuka zamani tulikuwa tunapata nafasi nyingi za kufunga lakini hatuzitumii, naona timu imebadilika kabisa, tumeanza kutumia nafasi chache tunazopata, na hasa za mipira ya faulo," alisema Hitimana.

Kocha huyo aliongeza kikosi hicho kilikuwa na wakati mgumu katika kutumia vizuri mipira ya faulo, lakini hali imekuwa tofauti katika mechi ya juzi, ambayo ilizalisha mabao mawili ya mipira hiyo.

Kaimu Kocha Mkuu wa KMC, Habib Kondo, alisema Simba haikuwazidi na wala haikuwashambulia sana kwa sababu wamepata mabao kwa njia ya faulo.

"Tumefungwa mabao matatu ya mpira wa kutengwa. Mara nyingi mabao ya mipira hiyo hayana ufundi kwenye kuzuia, mpira ukichukuliwa na kuingizwa ndani kama hamkuwa makini mnafungwa, nilivyoona ni bao moja tu ambalo halikuwa la faulo," alisema kocha huyo.

Wakati huo huo, Mshauri wa Mwekezaji wa Simba, Crescentius Magori, aliliambia gazeti hili wameshapokea ripoti ya Kocha Mkuu, Pablo Franco na itaanza kufanyiwa kazi rasmi kesho.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >